

MTAZAMO WA JAMII JUU YA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO 2014
KUHUSU KUTUMIA KISWAHILI KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA
ELIMU YA JUU KATIKA VYUO VYA KATI

VEDASTUS LUSATO GEREMU MUNUBI AMBROSE

TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA
MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI
YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2018

UTHIBITISHI

Niliyetia saina hapa chini ninathibitisha kuwa nimesoma tasnifu hii itwayo **Mtazamo wa Jamii Juu ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 Kuhusu Kutumia Kiswahili Kufundishia na Kujifunzia Elimu ya Juu katika Vyuvo vya Kati** na kupendekeza ikubaliwe kwa utahini na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya Masharti ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

.....
Sheikh, Profesa, Dkt. T. Y. M. K. S. Sengo

(Msimamizi)

.....
Tarehe

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile tasnifu hii kwa njia yoyote kama vile kielektroni, kurudufu nakala, kurekodi au kwa njia yoyote nyinginebila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa niaba

TAMKO

Mimi, Vedastus Lusato Geremu Munubi Ambrose, nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa Shahada kama hii au nyingine yoyote.

.....
Saini

.....
Tarehe

TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa mke wangu Getrude Migani Makene pamoja na wanangu Godwin Munubi, Prosper Makene, Ezekiel Nago, Gladness Nakataga na Nelson Gunje.

SHUKURANI

Kazi hii ni matokeo ya jitihada zangu binafsi pamoja na michango ya watu wengine. Sina budi kutoa japo neno la shukuranikwa wale wote walionishika mkono na kuniongoza katika safari hii ndefu katika uwanja huu wa taaluma.

Awali ya yote, ninatoa shukurani zangu za pekee kwa Mwenyezi Mungu ambaye amekuwa ni msaada mkubwa sana kwangu tangu nilipoanza kazi hii hadi kukamilika kwake. Ameniongoza na kunijaalia afya njema katika safari hii iliyojaa vikwazo vingina amenifanikishia ndoto yangu ya miaka mingi ya kupata shahada ya Uzamili katika Kiswahili.

Pili, ninatoa shukurani zangu za dhati kwa msimamizi wangu Sheikh, Profesa, Dkt, T.Y.M.K.S. Sengo kwa uongozi, uelekezaji, ukosoaji, ushauri na uvumilivu wake ambao umekuwa chachu ya kukamilisha kazi hii. Kwa hakika amenisaidiasana, amenijenga na kunikomaza kitaaluma na kitaalamu.

Tatu, shukurani zangu ninazitoa kwa Maprofesa na wahadhiri wote walionifundisha na kuniandaa kitaaluma hadi nikaweza kupata stadi za kuniwezesha kuikabili kazi hii. Shukurani hizi ni kwa Prof. James Mdee, Dkt. Elsifa Zelda, Dkt.Hanna Simpasa, Dkt Ligembe, Dkt. Kische na Dkt. Hadija Jilala bila kuwasahau kina Dkt. Hokororo, Mwalimu Sostenes Raphael Mashinji wa Chuo cha Ualimu Butimba.

Nne, nimshukru mke wangu Getrude Migani Makene pamoja na wanangu Godwin Munubi, Prosper Makene, Ezekiel Nago, Gladness Nakataga na Nelson Gunje kwa

sala na maombi yao pamoja na uvumilivu waliouonesha wakati wote walipokosa upendo wangu kutokana na kuhudhuria masomo ya kozi ya Uzamili.

Tano, shukurani zangu za dhati zimwendee Bwana Nteminyanda Kisabo kwa ushauri wake na kujitolea kwake muda wa kuchapa kazi hii tangu hatua za awali hadi kukamilika kwake.

Sita, nawashukuru wanafunzi wenzangu tuliokuwa nao katika safari ya kitaaluma 2015 / 2016 katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Nimefaidika na ushirikiano wao namichango yao imekuwa chachu katika kufanikisha kazi hii.

Mwisho, ninatoa shukurani kwa uongozi wa vyuo vya CBE na ADEM pamoja na wanafunzi wote walioshiriki katika utafiti huu.

IKISIRI

Utafiti huu ulilengakuchunguza mtazamo wa jamii juu ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 kuhusu matumizi ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya kati. Utafiti huu ulikuwa na madhumuni mahsusi matatu ambayo ni kubaini tamko la sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia, Kubainisha changamoto za utekelezaji wa sera ya Elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia, Kutoa mapendekezo juu ya utekelezaji wa sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya kijamii na utekelezaji. Utafiti huu ulifanywa katika wilaya za Nyamaganana Ilemela katika vyuo vya CBE na ADEM kwa kutumia watafitiwa 95 waliosailiwa na kujibu maswali. Watafitiwa waliteuliwa kwa kuzingatia kigezo cha nasibu na makusudi. Mbinu ya utafiti iliyotumika katika kukusanya data ilikuwa ni usaili, hojaji na utalii wa machapishi. Uchambuzi wa data zilizokusanywa umefanyika kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na kitakwimu. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa lugha ya Kiswahili inakidhi vigezo vyote vya kutumika kama lugha ya kufundishia na kujifunzia elimu katika vyuo vya kati. Matumizi ya lugha inayotumiwa na wazungumzaji wengi inaweza kuwa ni nyenzo muhimu katika kuinua ubora wa elimu itolewayo katika vyuo hivyo. Kutotumika kwa lugha ya Kiswahili kufundishia elimu nchini Tanzania hakuwasaidii wanafunzi kufikia viwango vinavyotakiwa. Aidha, hakuwasaidii kuendeleza vipaji na ubunifu wa wanafunzi katika kuikuza lugha ya Kiswahili ili iendane na mahitaji ya kutumika kufundishia na kujifunzia elimu ya kati.

YALIYOMO

UTHIBITISHI	ii
HAKIMILIKI	iii
TAMKO	iv
TABARUKU	v
SHUKURANI	vi
IKISIRI	viii
ORODHA YA MAJEDWALI	xiii
SURA YA KWANZA	1
1.0 UTANGULIZI	1
1.1 Utangulizi	1
1.2 Usuli wa Mada	1
1.3 Tatizo la Utafiti	5
1.4 Makusudio ya Utafiti.....	6
1.4.1 Lengo Kuu.....	6
1.4.2 Madhumuni Mahsusi.....	6
1.4.3 Maswali ya Utafiti.....	6
1.5 Umuhimu wa Utafiti	7
1.6 Mawanda ya Utafiti.....	7
1.7 Mipaka ya Utafiti	8
1.8 Vikwazo vya Utafiti	8
1.9 Mpangilio wa Tasnifu	9
1.10 Hitimishi.....	9

SURA YA PILI.....	11
2.0 UTALII WA MACHAPISHI NA MKABALA WA KINADHARIA	11
2.1 Utangulizi.....	11
2.2 Utalii Kuhusu Lugha ya Kufundishia na Kujifunzia Katika Elimu	11
2.3 Utalii wa Sera ya Lugha.....	14
2.3.1 Lugha Rasmi ya Kufundishia na Kujifunzia Tanzania	15
2.3.2 Sera ya Lugha ya Afrika Kusini.....	20
2.3.3 Sera ya Lugha ya Ghana	21
2.4 Utalii waUtafiti Uliyokwishafanyika	22
2.5 Pengo la Maarifa	32
2.6 Mkabala wa Kinadharia	32
2.6.1 Nadharia ya Kijamii	33
2.6.2 Nadharia ya Utekelezaji	34
2.7 Hitimisho.....	37
SURA YA TATU.....	39
3.0 MBINU ZA UTAFITI.....	39
3.1 Utangulizi.....	39
3.2 Mpango wa Utafiti	39
3.3 Eneo la Utafiti	39
3.4 Kundi Lengwa.....	40
3.5 Usampulishaji na Mbinu za Usampulishaji	40
3.5.1 Usampulishaji.....	40
3.5.2 Mbinu za Usampulishaji	41
3.6 Aina za Data Zilizo Kusanywa	42

3.6.1	Data za Msingi	43
3.6.2	Data za Upili	43
3.7	Mbinu za Utafiti	43
3.7.1	Mbinu za Kukusanya Data	43
3.7.2	Mbinu za Uchambuzi wa Data	45
3.8	Maadili ya Utafiti	46
3.9	Hitimishi.....	46
SURA YA NNE		47
4.0	UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA.....	47
4.1	Utangulizi.....	47
4.2	Sera ya Lugha ya Elimu na Mafunzo Kuhusu Kiswahili Kama Lugha Kufundishiana Kujifunzia	47
4.2.1	Uelewa wa Wadau wa Elimu Kuhusu Tamko la Kutumia Lugha ya Kiswahili	49
4.2.2	Uwazi wa Sera Kuhusu Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Kufundishia na Kujifunzia.....	52
4.3	Changamoto za Utekelezaji wa Sera.....	53
4.4	Mapendekezo	62
4.4.1	Mchango wa Lugha ya Kiingereza katika Kufundishia na Kujifunzia	62
4.4.2	Manufaa ya Kutumia Lugha ya Kiswahili katika Kufundishia naKujifunzia....	66
4.4.3	Athari ya Kutotekelezwa kwa Matamko ya Sera ya Elimu na Mafunzo Juu ya Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Kufundishia Vyuo vya Kati.....	68
4.4.4	Changamoto za Utekelezaji Tamko la Sera ya Elimu juu Yamatumizi ya Lugha ya Kiswahili Kufundishia na Kujifunzia Vyuo vya Kati	71

4.5	Hitimishi.....	75
	SURA YA TANO	76
5.0	MUHTASARI, HITIMISHI NA MAPENDEKEZO	76
5.1	Utangulizi.....	76
5.2	Muhtasari Kuhusu Utafiti.....	76
5.3	Matokeo ya Utafiti	78
5.4	Mapendekezo	80
5.5	Maeneo Yanayohitaji Utafiti Zaidi	82
5.6	Hitimishi.....	83
	MAREJELEO	84
	VIAMBATANISHO	91

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 3.1:	Idadi ya Uteuzi wa Watafitiwa.....	42
Jedwali 4.1:	Maoni ya Watafitiwa Kuhusu Tamko la Kutumia Lugha ya Kiswahili	49
Jedwali 4.2:	Majibu Yaliyotolewa na Watafitiwa Waliosema Wamesoma Ama Kusikia Tamko la kutumia Lugha Kiswahili	50
Jedwali 4.3:	Uwazi ya Sera ya Elimu Kuhusu Lugha ya Kiswahili Kufundishia na Kujifunzia.....	52
Jedwali 4.4:	Kutekelezeka Kwa Sera ya Elimu na Mafunzo Juu ya Kiswahili Kama Lugha Kufundishia na Kujifunzia	54
Jedwali 4.5:	Hatua Zilizochukuliwa na Serikali Kuhakikisha Matumizi ya Kiswahili	55
Jedwali 4.6:	Maoni ya Watafitiwa Kuhusu Mikakati ya Utekelezaji Iliyowekwa na Serikali	57
Jedwali 4.7:	Maoni ya Watafitiwa Juu ya Kutumia Lugha Kiswahili Katika Kufundishia na Kujifunzia	59
Jedwali 4.8:	Matumizi Yalugha ya Kiswahili ama Kiingereza Katika Mjadala ya Mada Wanazojifunza.....	61
Jedwali 4.9:	Maoni ya Watafitiwa Kuhusu Mchango wa Lugha ya Kiingereza Katika Kufundishia na Kujifunzia.....	63
Jedwali 4.10:	Maoni ya Watafitiwa Kuhusu Manufaa ya Kutumia Lugha ya Kiswahili katika Kufundishia na Kujifunzia	66

Jedwali 4.12: Maoni ya Watafitiwa Kuhusu Athari ya Kutotekelezwa kwa Tamko
la Matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika Kufundishia na Kujifunzia
katika Vyuo vya Kati..... 69

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Utangulizi

Sehemu hii inahusika na usuli wa mada, tatizo la utafiti, makusudi ya utafiti, madhumuni mahsusi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda na mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti na hitimishi.

1.2 Usuli wa Mada

Hoja ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia mfumo rasmi wa elimu ina historia ndefu nchini Tanzania. Ifahamike kuwa Tanzania ina lugha kati ya mia moja na ishirini na mia moja hamsini ambazo ni za jamii au asili. Kiswahili ni lugha inayozungumzwa na watu wengi kama lugha ya pili. Tafiti nyingi zinaonesha kuwashughulisha wataalam mbalimbali juu ya uteuzi wa lugha rasmi inayoweza kurahisisha mchakato wa kufundishia na kujifunzia katika muktadha kama wa Tanzania.

Kihistoria, kabla ya kuanzishwa kwa utawala wa kikoloni wa Wajerumani, wamisionari waliofika Tanganyika walianzisha shule. Mojawapo ya shule hizo ni ile iliyojengwa Mpwapwa mwaka 1876 kwa lengo la kuwafunza wafuasi wao. Wamisionari hao walitumia Kiswahili na lugha za wenyeji wao katika kutolea elimu (Gottneid, 1976). Wao waliamini kuwa lugha huwasilisha fikra za watu, utamaduni na mifumo ya utawala katika jamii hizo. Hivyo, namna bora narahisi ya kuelewa mila na dasturi za jamii ni kupitia lugha zao. Kiswahili kilikuwa

mojawapoya lugha iliyozungumzwa na wenyeji wa Tanganyika kama lugha ya pili (Morrison 1971).

Hata hivyo suala la lugha ya kufundishia nchini Tanzania limekuwa na mjadala mrefu ambapo tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusu ni lugha gani inapaswa kutumika katika kufundishia kati ya Kiswahili na Kiingereza. Kwa mujibu wa UNESCO (1953), Lugha za jamii ni bora katika kufundishia kuliko zile za kigeni kwa sababu kiushunuzi, lugha ya jamii ni mfumo wa alama zenye maana ambazo katika akili ya mwanafunzi hufanya kazi haraka katika kuelewa na kujieleza. Kiushunuzi, lugha ya mtu ni njia ya kujinasibisha na jamii yake. Kielemu, mwanafunzi hujifunza kwa haraka kwa kutumia lugha anayoielewa kuliko lugha ngeni. Mfano, lugha ya Kiswahili ina mizizi sawa na lugha za kienyeji kama vile Kikwere, neno mama ni mama kama lilivyo katika Kiswahili.

Kutokana na maelezo hayo, inaonesha kuwa, upo umuhimu wa kutumia lugha yenye nasaba na lugha za asili katika kufundishia na kujifunzia. Kwa Tanzania, Kiswahili, ni lugha ya taifa na inayokidhi kuwa lugha ya pili kwa jamii pana ya Watanzania. Pamoja kuwa Kiswahili si lugha ya jamii kwa Tanzania, lakini ni lugha inayozungumzwa na Watanzania wengi na hata kuwa lugha ya kwanza kwa baadhi ya watu. Hivyo, matumizi ya Kiswahili kufundishia ngazi zote za elimu yatawezesha wanafunzi kujinasibisha na jamii zao za Kitanzania na kurahisha kujifunza maarifa mapya kwa kuondoa kikwazo cha lugha ya mawasiliano katika muendeleo wa kufundisha na kujifunza. Walimu watafundisha maarifa mapya kwa lugha wanayoifahamu.

Wakati wa utawala wa Wajerumani, walianzisha shule nyingi katika utawala wao kuleTanga, mwaka 1892 (Gottneid, 1976) na Bush schools nyingi vijijini. Kiswahili kilitumika katika kufundishia ngazi za chini za Elimu ya Msingi hasa katika Shule za Waafrika (Whiteley, 1969). Kiswahili kilitumika pia kama lugha ya shughuli za kiutawala (Gottneid, 1976).Mtaalam huyu anaendelea kufafanua kuwaWajerumani walisisitiza kila akida na kila jumbe kukifahamu Kiswahili ili waweze kufanya kazi mahali popote kwa lengo la kutekeleza shughuli za kiutawala.Zuri moja na kubwa walilofanikiwa kulifanya wakoloni hao ni kukikuza na kukiendeleza Kiswahili ingawa lugha yenyewe, kwa asili yake, ina nguvu zake yenyewe ya kujitanua na kujipeleka mbele.

Aidhani, utawala wa Waingereza (1919 -1961) uliweka msisitizo katika matumizi ya lugha yao ya Kiingereza katika mfumo wa elimu.Waingereza walitumia pia Kiswahili katika kufundishia ngazi za chini za elimuhususan katika Shule za Waafrika kuanzia darasa la I hadi IV. Kiingereza kilitumika kuanzia darasa la tano hadi la nane katika shule za kati na shule za juu za msingi. Matokeo ya hali hiyo ni kwamba ujuzi wa lugha ya Kiingereza ulifasiliwa kuwa ndiyo ishara ya kuelimika.Watu wengi hadi leo bado wanayo kasumba ya kukitaka Kiingereza iliwaonekane wameelimika bila ya kuzingatia kwambaKiingereza siyo kigezo pekee cha elimu.

Wakati wa kupigania uhuru na baada ya uhuru (1954–1964), lugha ya Kiswahili iliyotumiwa na watu wengi ilituuliwa kuwa lugha ya Taifa na hatimaye ikawa lugha rasmi (Kiango, 2002). Tangu kipindi hicho (1961 – 1964) hatua mbalimbali

zilichukuliwa za kukuza na kuimarisha Kiswahili ili kukiwezesha kutumika katika kufundishia elimu ya ngazi zote. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na kuasisiwa kwa Elimu ya Kujitegemea mwaka 1967 ambapo Kiswahili kilitangazwa rasmi kuwa ni lugha ya kufundishia katika shule zote za msingi na somo la lazima katika sekondari zote za serikali. Kwa hali hiyo, mfumo mpya wa lugha ya kufundishia ulianzishwa rasmi. Mhina (1972) aliitolea ufafanuzi kauli hiyo kwa kusema:

“Huu ulikuwa mwamko mpya wa kifikra katika elimu kwa mamlaka za serikali kwamba, elimu sahihi kwa wanafunzi wetu wa shule za msingi ni ile iliyotolewa kwa kutumia lugha ya Kiswahili waliyoifahamu vizuri zaidi kuliko Kiingereza” (tar- jama yangu)

Mabadiliko hayo ya lugha ya kufundishia katika Shule za Msingi yalichochea pia mabadiliko ya lugha ya kufundishia katika vyuo vya ualimu. Kiswahili, kilianza kutumika mwaka 1970 kufundishia masomo yote katika Shule za Msingi isipokuwa somo la Kiingereza tu.

Matarajio yalikuwa ni kupanua na kujumuisha shule za upili na hatimaye vyuo vikuu. Hata hivyo, kufikia mwaka 1984, serikali ilitoa tamko kuwa Kiingereza kiendeleo kutumika (Msanjila, 2009). Tamko hilo liliyumbisha tamaa na matumaini ya waendelezaji wa Kiswahili.

Pia, ripoti ya Tume ya Rais ya Elimu ya mwaka 1982 iliyojulikana kwa jina la Tume ya Makweta ilishauri Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia elimu ya juu nchini Tanzania kuanzia shule za upili ifikapo 1985 na vyuo vikuu ifikapo 1992.

Aidhani, Sera ya Utamaduni (Wizara ya Elimu, 1997) ilibainisha mipango iliyofanywa ya kukiwezesha Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katika ngazi zote

za elimu. Vilevile sera ya Elimu na Mafunzo (Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, 2014) ilitamka bayana kuwa lugha ya Taifa ya Kiswahili ingetumika kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na mafunzo. Serikali ingeweka utaratibu wa kuwezesha matumizi ya lugha hiyo kuwa endelevu na yenye ufanisi katika kuwapatia walengwa elimu na mafunzo yenye tija kitaifa na kimataifa. Kwa kuzingatia maelezo hayoni dhahiri kuwa kumekuwapo na hatua, mipango na sera anuai zenye kujenga matumaini ya kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia ngazi zote za elimu.

Hata hivyo, mpaka sasa matumizi ya Kiswahili kufundishia bado yanafanyika katika ngazi ya elimu ya awali, elimu ya msingi na vyuo vya ualimu ngazi ya Stashahada yakawaida. Kutokana na hali hiyo, utafiti huu utajikita kuchunguza mtazamo wa jamii juu ya sera ya Elimu na Mafunzo 2014 kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati ili kuona jinsi ambavyo sera hiyo inatekeleza ama la.

1.3 Tatizo la Utafiti

Tatizo la kukosekana kwa lugha yenyeji ya kubeba mzigo wa maarifa, elimu ya kuikomboa Tanzania kuondokana na utumwa wa kasumba ya lugha ya Kiingereza ni la zamani sana. Kwa kuzingatia maandishi yaliyotaliwa, inaonekana kazi nyingi na kubwa zilikwishafanyika kuhusu lugha ya kufundishia katika mfumo wa elimu Tanzania kwa nyakati tafauti kama ilivyobainishwa katika usuli. Utafiti huo mwingi ulijikita katika shule za sekondari, vyuo vya ualimu na vyuo vikuu. Kwa muktadha huo, mtafiti ameamua kufanya utafiti huu, baada ya kugundua kwamba licha ya

kuwapo kwa matamshi yaliyohusu Sera ya Elimu na Mafunzo (1995), Sera ya Utamaduni (1997), na Sera ya Elimu na Mafunzo (2014) ambazo zimebeba ujumbe juu ya matumizi ya Kiswahili kufundishia ngazi zote za elimu, bado kuna kigugumizi katika utekezaji wake. Kwa mantiki hiyo, mtafiti ameamua kufanya utafiti kwa lengo la kuchunguza mtazamo wa jamii juu ya sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka (2014) kuhusu matumizi ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu ngazi zote za elimu.

1.4 Makusudio ya Utafiti

1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza mtazamo wa jamii juu ya sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka (2014) kuhusu matumizi ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Kati.

1.4.2 Madhumuni Mahsusi

- i) Kubainisha tamko la sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili Kama lugha ya kufundishia na kujifunzia elimu katika Vyuo vya Kati.
- ii) Kubainisha changamoto za utekezaji wa sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia
- iii) Kutoa mapendekezo juu ya utekezaji juu ya sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia

1.4.3 Maswali ya Utafiti

- i) Je tamko la sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia linasema nini?

- ii) Je kuna changamoto gani katika utekelezaji wa sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia?
- iii) Je nini kifanyike ili sera yaelimu kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia iweze kutekelezeka?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Kwanza, utafiti huu unatoa mchango katika matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufundisha na kujifunza elimu katika Vyuo vya Kati. Hivyo, kwa kusoma kazi hii, jamii itaelewa matatizo na athari za lugha za kufundishia na kujifunzia katika utoaji wa elimu bora. Pili, utafiti umechochea watafiti wengine kutafiti juu ya mada hii kwa kutumia maeneo mapana zaidi, na utafiti huu ukitumiwa kama marejeleo kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili, kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika Vyuo vya Kati, kwa watafiti wengine. Tatu, utafiti unaamsha ari mpyakwa Serikali, kuamua, namna nzuri ya kutekeleza uamuzi wa kutumia Kiswahili kufundishia elimu, ngazi ya Vyuo vya Kati. Vivyo hivyo, utafiti umesaidia wahitaji wa elimu kupata maarifa na ujuzi mpya kwa matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya Vyuo vya Kati.

1.6 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza mtazamo wa jamii juu ya sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka (2014) kuhusu matumizi ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Kati. Utafiti haukuhusisha viwango vingine vya elimu, kama vile, Sekondari na Vyuo Vikuu, kwa sababu maeneo hayo hayakulengwa na mtafiti. Aidhani, utafiti huu ulihusisha Vyuo vya Kati vya CBE na ADEM vilivyopo

katika Wilaya ya Nyamagana na Ilemela, mkoani Mwanza, kwa vile viko karibu na eneo analoishi mtafiti na ndivyo vyuo ambavyo mtafiti amevilenga katika utafiti huu.

1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza Siri zinazoizunguka sera ya lugha, ya Kiswahili, kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati. Katika kufikia kusudio hilo, kulizingatiwa uwazi wa sera ya lugha ya Kiswahili katika ufundishaji na kujifunzia, matatizo yanayokwamisha utekelezaji wa matumizi ya Kiswahili katika wa kufundishia na kujifunzia pamoja na athari zitokanazo na matumizi ya lugha ya kufundishia na kujifunzia katika utoaji wa elimu bora. Hata hivyo, Utafiti ulijikita katika kuchunguza mtazamo wa jamii juu ya sera ya Elimu na Mafunzo yam waka 2014 kuhusu kutumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia katika vyuo kati, aidha ni, utafiti uliwalenga wanachuo na wahadhiri pamoja na wakereketwa wa elimu kamavile maafisa elimu na wathibiti ubora wa elimu, watunga sera na wanasiasa

1.8 Vikwazo vya Utafiti

Vikwazo katika utafiti kwa namna yoyote haviwezi kuepukika. Kwa mujibu wa Durrel (1987) vikwazo katika utafiti ni vitu au mambo ambayo hukwaza mchakato wa uendeshaji wa utafiti.

Katika kipindi cha utafiti, hususani wakati wa ukusanyaji wa data, mtafiti alikumbana na vikwazo mbalimbali kutoka masikanini. Kwa vile utafiti huu ulihusisha zaidi jamii ya watu waliokuwa wakitumia Kiingereza katika kufundisha na

kujifunza, ilimlazimu mtafiti kupokea mtazamo yao tu juu ya matumizi ya Kiswahili katika tendo la upokeaji wa elimu kwa sababu hapakuwa na vyuo vya elimu ya kati vinavyoendesha mafunzo yake kwa Kiswahili. Kikwazo kingine ni baadhi ya watafitiwa kuomba fedha kutoka kwa mtafiti. Hii inatokana na Imani miongoni mwa wanajamii kuwa mtafiti amefadhiliwa kufanya utafiti wake hivyo wao hawaoni kama kuna faida kwao na hivyo huona ni vizuri jasho lao kulipiwa ili kutoa data. Kuondokana na kadhia hii, mtafiti alilazimika kutoa elimu kwa walewaliokuwa tayari kutoa data na hivyo kufanikiwa kupata data kwa ajili ya utafiti huu. Kikwazo kingine ilikuwa ni gharama iliyohusisha rasilimali fedha ikiwa ni nauli ya kusafiri mpaka Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam kwa ajili ya huduma ya maktaba. Mtafiti alikabiliana na changamoto hiyo kwa kutumia mapato yake binafsi.

1.9 Mpangilio wa Tasnifu

Muundo wa tasnifu hii umegawanyika katika katika sura tano; ya kwanza ni utangulizi wa jumla wa utafiti uliohusu masuala yanayohusiana na tatizo lililofanyiwa uchunguzi. Sura ya pili inahusu utalii wa kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti, ukusanyaji data, uteuzi wa wawakilishi wa utafiti na mkabala uliotumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu. Sura ya nne inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data na sura ya tano inahusu muhtasari wa matokeo, hitimishi na mapendekezo.

1.10 Hitimishi

Sura hii inatoa picha ya usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti na

utatuzi wake nampangilio wa tasnifu. Katika sura ya kwanza, tatizo la utafiti limebainishwa na kuelezwa wazi na kwa undani zaidi. Sura inayofuata inahusu utalii wa maandishi tangulizi yenye kuhusiana na kazi yetu ambayo yalisaidia katika kufikia lengo la utafiti huu.

SURA YA PILI

2.0 UTALII WA MACHAPISHI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu usomaji wa mzamo wa machapishi yanayohusiana na mada ya utafiti pamoja na mkabala wa nadharia uliyotumika. Katika usomaji wa machapishi yaliyohusiana na mada ya utafiti, kumejadiliwa kwa kina hoja zote za msingi na hatimaye kuibua pengo la maarifa ambalo limeweka msukumo wa kufanya utafiti huu. Machapishi hayo ni utalii kuhusu lugha ya kufundishia na kujifunzia katika elimu na utalii wa sera ya Elimu. Pia tumegusa mkabala wa kinadharia ambapo tumefafanua misingi ya nadharia zilizotumika katika uchambuzi wa data.

2.2 Utalii Kuhusu Lugha ya Kufundishia na Kujifunzia Katika Elimu

Lugha ya kufundishia ni lugha iliyoteuliwa kutolea elimu kwa taifa nzima au sehemu ya taifa na kwa kiwango maalum cha elimu au kwa viwango vyote vya elimu. Hoja hiyo inaungwa mkono na Msanjila na wenziwe (2009) waliposema kwamba lugha ya kufundishia ni lugha inayotumiwa kutolea maarifa katika mfumo wa elimu. Lugha hiyo ndiyo inayotumika kujenga mfumowa mawasiliano katika elimu ya msingi kwa umma, kubuni na kuendeleza maarifa. Wanaendelea kueleza kuwa lugha ni chombo cha kuwapa watu uwezo na nguvu za kiutamaduni na kiulimbe. Kwa mtazamo wao lugha ya kufundishia ina dhima kubwa katika maendeleo ya jamii kwa kukuza fikra pevu zilizo msingi wa ubunifu na ugunduzi. Akiunga mkono hoja hii, Besha(1999) anaeleza kwamba matumizi ya lugha ya kufundishia katika mfumo wa elimu licha ya

kuwasaidia wanafunzi kuendeleza vipaji vyao vya ubunifu,huwa pia ndiyo njia pekee ya kuendeleza lugha hiyo katika kukabiliana na taaluma za ulimbe na utunduizi.

Senkoro (2004) anashadidia kuwalugha ifaayo kufundishia ni ileinayoeleweka vizuri kwa walimu na wanafunzi.

Kwa mujibu wa Prah (2003), lugha ya kufundishia ni ile yenye athari kubwa katika mfumo wa elimu;ninyenzo itumikayo kujenga mfumo thabiti wa elimu na huwa na nguvu na mamlaka kwa kuwa dhana kuu za elimu tayari zimo kwenye lugha hiyo ya asili, au ya karibu, kama kilivyo Kiswahili kwa Watanzania wengi. Mwanafunzi hujifunza geni moja tu la elimu na si mageni mawilikwa maana yalugha na elimu.

Tanzania inapoendelea kuenzi na kutumia lugha ya kigeni kufundishia kama vile Kiingereza, ambazo hazifahamiki na hazitumiki katika jamii pana za watanzania uhuru wa kiutamaduni hauwezi kupatikana kwa urahisi.

UNESCO (1953)kwa upande wake inaona kuwa lugha za jamii ni bora katika kufundishia kuliko lugha zote za kigeni. Inabainisha sababu tatu kama ifuatavyo;moja, lugha ya jamii ni mfumo wa dhanaa zenye maana kwao ambazo katika akili ya mwanafunzi hufanya kazi haraka katika kujielezeka na kueleweka. Mbili,lugha ya mtu ni njia ya kujinasibisha na kwao. Tatu ni sababu ya kielimu ambayo kwayo mwanafunzi hujifunza haraka kupitia lugha anayoelewa vema kuliko lugha ngeni. “Lugha mama” humfanyakama ilivyosemwa hapo juu. Mwanafunzi ajifunze kigeni kimoja, maarifa tu badala ya lugha ngeni na maarifa mageni.

Kwa kawaida, katika jamii huru kisiasa, kiuchumi, na kiutamaduni, utoaji wa elimu hufanywa kwa kutumia lugha iliyoteuliwa rasmi miongoni mwa lugha nyinginezo kama Kiswahili kilivyopendekezwa. Kwa mazingira ya Tanzania, Kiswahili ndiyo lugha ya pili inayozungumzwa na watu wengi zaidi ikilinganishwa na lugha nyingine zipatazo kati ya mia ishirini na mia hamsini. Kwa sababu hiyo basi, Kiswahili kinaweza kupewa dhamana ya kuweza kutumika kukidhi haja ya kufundishia na kujifunzia elimu yenye manufaa kwa jamii. Kigezo kingine ni kwamba Kiswahili ni lugha ya Kibantu yenye mfumo unaofanana na lugha nyingine nyingi za Kitanzania. Tunaweza kuthibitisha hoja yetu kwa mifano ya maneno machache kama vile: koko (Kikwere)-boga-maboga (Kiswahili).

Kuchangia mjadala huu, Brock-Utne (2003) anadai kuwa lugha zinazotumika kufundishia katika madarasa ya Afrika ni lugha ambazo hazitumiwi na wanafunzi wawapo nje ya shule na wala hawaiielewi kwa usahihi. Katika utafiti huu, hoja hii inarejelea matumizi ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia elimu katika vyuo vya elimu vya kati. Anakwenda mbele zaidi na kubainisha kuwa walimu wenyewe hawatumii lugha hiyo nje ya mazingira ya darasa. Kwa hali hiyo basi, wanafunzi wa Tanzania hupoteza ujuzi wa Kiingereza mara tu wanapokihitimu kisomo chao kwa sababu jamii inayowazunguka haitumii lugha hiyo katika shughuli zao za kila siku (Rubanza, 2002).

Kwa jumla, lugha ya kufundishia inapaswa kuwa ni ile inayotumiwa na watu wengi katika mawasiliano yao ya kila siku kama ilivyo kwa Kiswahili. Ikitumika lugha hiyo itafungua milango ya kupitishia maarifa kutoka kwa mwalimu kwenda kwa

mwanafunzi, kwenda kutumika na jamii huwa ndicho chombo cha kumwezesha mwanafunzi kung'amua, kuelezana kutekeleza hisia zake zandani kwa kile kinachomfikia au kinachotoka moyoni mwake (Qorro, 2000).

2.3 Utalii wa Sera ya Lugha

Rubin na Jernudd (1971) wanaifafanua sera ya lugha kuwa ni jumla ya matukio, shughuli, au hatua za wazi na fiche zinazochukuliwa na dola kwa makusudi ya kuleta au kusitisha mabadiliko katika jamii. Mekacha (2000) kwa upande wake anaidavua sera ya lugha kama jumla ya mawazo, matamko, sheria, kanuni na taratibu zenye kuelezea taratibu za utekelezaji wa mabadiliko ya nafasi na matumizi ya lugha katika jamii. Sera ya lugha inapaswa kuzingatia na kutamka mambo ya msingi yafuatayo; namna lugha mbalimbali katika jamii ziinavyopaswa kutumika kikamilifu, namna ya kujenga stadi za lugha zitakiwazo ili kukidhi mahitaji ya vipaumbele vya taifa na namna ya kutetea haki za watu, makundi ya jamii yanayotaka kujifunza na kudumisha lugha zao (Msanjila, 2009). Kutokana na mawazo hayo, tunaweza kusema kuwa sera ya lugha ni mwongozo wa kusimamia matumizi ya lugha katika jamii au nchi na serikali ndiyo yenye dhamana ya kuandaa aina ya sera inatokidhi matakwa ya jamii husika.

Dhana ya sera ya lugha ina uhusiano mkubwa na dhana ya mpango wa lugha kiutendaji. Mpango lugha ni jumla ya matukio, shughuli au hatua za wazi na zisizo za wazi zinazochukuliwa na dola kwa makusudi ya kuleta mabadiliko au kusitisha mabadiliko yasiendeleo kutokea katika jamii kuhusiana na taratibu za matumizi ya lugha (Kaplan na Baldauf, 1997).

Kwa jumla, sera ya lugha huwa na mipango lugha mingi inayotakiwa kutekelezwa. Kwa mfano, mpango lugha unaolenga kukuza na kuendeleza lugha za kikabila zitumike katika kufundishia. Kaplan na Baldauf (wameshatajwa) wameainisha sera za lugha katika makundi mawili ambayo ni sera halisi za lugha na sera za kiishara. Sera halisi ni sera za maandishi ambazo maelezo yake yameandikwa katika kijitabu ambacho kimejadiliwa na kupitishwa na vyombo rasmi vya kiutawala katika nchi inayohusika. Sera za kiishara ni jumla ya matamko, kauli au nyaraka ambazo zipo kwa ajili ya kukidhi matakwa ya kisiasa. Wazaramo wana maneno yao, “zilongwa mbali, zitendwa mbali.” Maana ya maneno ya maneno ni kwamba yanayosemwa kuhusu Kiswahili, na vitendo hutendewa Kiingereza kwenye taifa letu la Tanzania.

2.3.1 Lugha Rasmi ya Kufundishia na Kujifunzia Tanzania

Mchakato wa kutafuta lugha rasmi ya kufundishia na kujifunzia nchini Tanzania unaweza kutazamwa kihistoria katika vipindi viwili ambavyo ni kabla na baadaya uhuru. Katika utawala wa Wajerumani (1887- 1918) matumizi ya Kiswahili yalihimizwa (Gottneid, 1977). Walitumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia elimu ya msingi (Whiteley, 1969).

Utawala wa Waingereza (1919 -1961) uliendeleza Kiswahili kama lugha ya kufundishia elimu ya msingi kuanzia darasa la kwanza hadi la nne. Kuanzia darasa la tano, Kiingereza kilitumika kufundishia masomo yotena Kiswahili kikabaki kuwa somo la lazima katika miaka mine (4) ya shule za kati na miaka mine (4) mingine kwa elimu ya sekondari. Jambo la msingi lililofanywa na utawala wa Waingereza ni kughushi lugha ya Kiswahili. Kitendo hicho kilibadilisha Kiswahili fasaha kuwa

Kiswahili kipa cha shule (kisanifu) na kupotosha matumizi ya lugha asilia inayojihirisha kwenye lahaja za Kiswahili mfano kimtang'ata kitumbatu (Sengo, 2017).

Wakati wa uhuru, kati ya miaka ya 1967 hadi 1987, elimu ya Tanzania ilifuata itikadi ya Ujamaa na Kujitegemea. Mabadiliko ya itikadi toka ubepari kuwa ya Ujamaa kuliambatana na mabadiliko makubwa katika mfumo wa elimu. Katika utekezaji wa itikadi hiyo katika mfumo wa elimu, kulianzishwa elimu ya kujitegemea. Kiswahili kilifanywa kuwa lugha ya kufundishia katika elimu ya msingi kwa sababu ilikuwa inazungumzwa na watu wengi. Lengo la elimu ya kujitegemea lilikuwa ni kuwawezesha wanafunzi kujitegemea baada ya kumaliza elimu ya msingi. Ukweli wa lengo hilo ulifahamika na wahitimu wote wa shule za kati. Hatua hiyo ya kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katika ngazi za shule za msingi ilikuwa ndani ya mpango mkubwa wa utekezaji wa Kiswahili kukifanya kuwa lugha ya kufundishia ngazi zote za elimu (Brock-Utne, 2000). Hayo, yalitokana na tamko rasmi la aliyekuwa Waziri Mkuu wa wakati huo, Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa. Alikusudia kufanya Kiswahili kitumike pote na kwa wote ikiwa na maana kwa Watanzania na wageni. Ni katika kipindi hicho ndipo mwalimu Siwale wa Mzumbe alitafasiri *Boxing, kwa Ngumi za Masanduku* (Sengo, 2017).

Brock- Utne (2000) wanadadai kuwamwaka 1969 Wizara ya Elimu ya Taifa ilitoa waraka kwa wakuu wote wa shule za sekondari, ikiwataka kuanza utekezaji wa kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia. Kwa mujibu wa Bhaiji (1976) walimu wengi wa shule za sekondari walitafiki hoja ya kukifanya Kiswahili kuwa

lugha ya kufundishia. Waraka huopia ulipendekeza kuwa somo la siasa linapaswa kufundishwa kwa lugha ya Kiswahili kuanzia 1969 / 1970, Sayansi Kimu 1970 /1971, Historia, Jiografia, Biolojia, Kilimo na Hisabati kuanzia 1971, 1972 (Bhaiji, 1976). Mpaka kufikia hatua hiyo, tafiti zote hazioneshi kuwa serikali ilitoa sera ya matumizi ya lugha inayojitegemea katika ufundishaji na ujifunzaji katika vyuo vya elimu vya kati.

Bhaiji (keshatajwa) anaendelea kubainisha kuwa wakuza mitala walishaanza kutarijamuna kukusanya istilahi za masomo ya Sayansi na Hisabati. Katika kipindi hicho baadhi ya shule za Sekondari zilikwishapata kijitabu chenye istilahi za Hisabatikatikalugha ya Kiswahili. Miaka ya mwishoni mwa 1970 ilishuhudia kuibuka kwa mjadala mkali kuhusu kutumia Kiswahili kufundishia ngazi zote za elimu. Mjadala huo umedumu hadi leo. Kutokana na mjadala huo, maoni ya kufuja wazo la kuitumia lugha ya kufundishia nchini Tanzania yaligawanyika katika pande mbili: wale waliokubali kuwa Kiswahili kitumike kufundishia ngazi zote za elimu na wale waliopinga na kushadidia kukifanya Kiingereza kiendeleo kutumika katika ngazi zote za elimu.

Aidhani, Tume ya Rais ya mwaka 1982 ilipendekeza Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katikangazizote za elimunchini Tanzania (United Republic of Tanzania, 1984). Mapendekezo hayo hayakutekelezwa mpaka leo. Kiingereza kiliendelea kuwa lugha ya kufundishia na kujifunzia katika elimu ya juu na Kiswahili kikabaki kuwa lugha ya kufundishia na kujifunzia Elimu ya Msingi, Elimu ya Cheti cha Ualimu (Grade A) na somo katika shule za sekondari na vyuo vikuu.

Kuanzia, miaka ya 1987, nchi ilianzisha sera ya soko huru. Sera hiyo iliambatana na ubinafsishaji wa njia kuu za uzalishaji mali. Mabadiliko hayo yaliathiri mfumo wa elimu pia. Miaka ya 1990 ilishuhudia ongezeko la shule binafsi za Msingi na za Sekondari. Katika kipindi hicho Serikali ilipitisha marekebisho ya kanuni ya Elimu ya mwaka 1995. Shule binafsi za msingi ziliruhusiwa kutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia ilihali shule za msingi za serikali zikiendelea kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia. Hali hiyo ilidhihirisha namna nchi isivyokuwana sera ya lugha thabiti inayojitegemea isipokuwa kuna nyaraka zenye miongozo na sera zilizobeba ujumbe wa matumizi ya lugha.

Kama ilivyobainishwa huko nyuma, Tanzania haina sera inayojitegemea juu ya lugha na lugha ya kufundishia. Matamko yanayohusu matumizi ya lugha na lugha ya kufundishia yanapatikana ndani ya Sera ya Elimu na Mafunzo (1995), Sera ya Utamaduni (1997) na Sera ya Elimu na Mafunzo (2014). Hali hiyo inadhihirisha madai ya Bamgbose (1991) kuwa sera ya lugha katika nchi nyingi za Afrika ni sera za ishara ambazo zimebaki kuwa matamko au maazimio yenye nia ya kufanya mabadiliko lakini maazimio hayo hayatekelezeki. Tanzania, kama zilivyo nchi nyingine za Kiafrika, inatumia sera za kiishara ambazo zimo ndani ya mlolongo wa nyaraka za serikali na matamko ya viongozi yanayohusu kutumia au kutokutumia lugha ya Kiswahili au Kiingereza katika baadhi ya maeneo rasmi ya matumizi ya lugha na yale yanayohusu taratibu za kukuza na kuendeleza lugha (Coulmas 1989).

Matamko kuhusu lugha ya kufundishia yaliyomo katika sera zilizokwishatajwa yana ukinzani wa kimawazo kama asemavyo Burchert (1997) kwamba wakati sera ya

Elimu na Mafunzo (1995) ikitangaza kwamba Kiingereza kitaendelea kuwa lugha ya kufundishia katika elimu na mafunzo ya ngazi za juu, Sera ya Utamaduni (1997) inatamka kwamba mipango itafanywa ya kukiwezesha Kiswahili kutumika kama lugha ya kufundishia katika Elimu na Mafunzo ya ngazi zote. Tofauti na zilizotangulia Sera ya Elimu na mafunzo (2014) inatamka kuwa lugha ya Taifa Kiswahili itatumika kufundishia ngazi zote za Elimu na Mafunzo na Serikali itaweka utaratibu wa kuwezesha matumizi ya lugha hiyo kuwa endelevu na yenye ufanisi katika kuwapatia walengwa elimu na mafunzo yenye tija kitaifa na kimataifa. Sera hiyo inaendelea kubainisha kuwa serikali itaendelea kuimarisha matumizi ya lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia elimu katika ngazi zote za Elimu na Mafunzo. Ni miaka mitatu sasa tangu kuzinduliwa kwake na bado lugha ya Kiswahili haijapewa fursa ya kutumika kufundishia katika elimu ngazi zote. Ugumu uko wapi wa kutekelezwa?

Mekacha (2000) na Msanjila (2009) wanajenga hojakuwa sera ya lugha Tanzania haiwiani na muktadha walughawiya jamii inamopaswa kutumika katika mfumo waelimu ya msingi ambapo lugha ya kufundishia elimu ya Sekondari na elimu ya juu ni Kiingereza. Lugha ya Kiswahili imeenea kote Tanzania lakini haitumiki kama lugha ya kufundishia. Lugha ya Kiingereza haifahamiki kwa walimu na wanafunzi wengi lakini bado imeshikiliwa kufundishia elimu na mafunzo ya ngazi za juu. Kimsingi, sera ya lugha haikidhi haja na matakwa ya wanajamii kwa kuzingatia mahitaji ya sasa ya Kiswahili ndani na nje ya nchi. Ujumbe wa matumizi ya lugha ya Kiswahili unaobebwa na sera zilizobainishwa, hauzingatii shughuli za ushirikiano wa kikanda na kimataifa kwa kuwa Kiswahili ni moja ya lugha rasmi shughuli za

ushirikiano wa kikanda na wa kimataifa kwa kuwa Kiswahili ni moja ya lugha rasmi katika mikutano ya Bunge la Afrika Mashariki, Bunge la Afrika na Umoja wa Afrika. Hivyo, inatakiwa lugha ya Kiswahili itumike kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vyetu ili kukidhi mahitaji yaliyopo sasa katika jamii. Kiingereza ndiyo bidhaa kubwa iliyobaki katika uchumi wa Waingereza. Tanzania ingejifunza kuipatia faida bidhaa (Kiswahili) kabla haijanyang'anywa na nchi jirani ambayo imeanza kula matunda hayo kwa kuwahitimishia wanachuo zaidi ya 1000 kila mwaka washahada ya kwanza ya Kiswahili, zaidi ya wanachuo 500 shahada ya Uzamili (M. A) na zaidi ya 300 shahada ya Uzamilivu (PhD). Wakitakiwa wataalamu duniani wenye sifa hizo ni Wakenya.

2.3.2 Sera ya Lugha ya Afrika Kusini

Sera ya lugha ya Afrika Kusini iko tafauti na hii ya Tanzania. Nchi ya Afrika Kusini ina lugha nyingi. Kuwapo kwa lugha nyingi Afrika Kusini kunalindwa na Katiba (Bamgbose 2003) ambayo inatoa haki kwa wananchi wake kutumia lugha 11 zinazotumiwa na asilimia 98 ya wananchi wa nchi hiyo. Katiba ya nchi hiyo inatamka bayanakwamba:

Kwa makadirio, kuna kama lugha 25 zinazozungumzwa Afrika Kusini ambapo kati ya hizo, lugha 11 zimepewa hadhi ya kutumika kiofisi kwa mujibu wa kipengele cha 6 cha Katiba (Ibara ya 108 ya mwaka 1996), katika mazingira kwamba matumizi ya lugha hizo yanajumuisha kama asilimia 98 ya watu wote wa Afrika Kusini (Tar-jama yangu).

Katiba ya nchi hiyo inaeleza wazi kuwa kila mtu ana haki ya kupata elimu kwa kutumia lugha rasmi yoyote aliyoichagua. Lugha rasmi hizo 11 ni Kiafrikana, Kiingereza, Kizulu, Kisepedi, Kisotho, Kiswana, Kiswati, Kivemba, Kitsonga, Kixhosa na Kindebele. Katiba ya Afrika Kusini inaheshimu jamii kutumia lugha zao

ambazo ni rasmi na kuheshimu tamaduni zao na inaeleza wazi kuwa kilamtu anayo haki ya kujitetea, kutoa ushahidi na kushtakiwa kwa kutumia lugha anayoifahamu.

Sera ya lugha ya Afrika Kusini inaonekana ni tafauti na ujumbe wa matumizi ya lugha unaobebwa na sera mbalimbali za Tanzania kama zilivyobainishwa huko nyuma. Baadhi ya sifa bainifu za sera ya lugha ya Afrika Kusini ni kama ifuatavyo: moja, inalindwa na Katiba ya nchi hiyo ambayo inatoa haki ya kupatiwa elimu wananchi wake kwa kutumia lugha zao ambazo ni rasmi. Matumizi hayo yanawasaidi wananchi kuelewa elimu wanayojifunza shuleni na vyuoni, tafauti na ambavyo wangependishwa kwa lugha za kigeni ambazo hawazielewi. Pili, sera ya lugha ya Afrika Kusini inajitegemea. Tatu, ina matamko yanayotekelezeka kwa sababu inalindwa na katiba ya nchi, tafauti kabisa na ujumbe wa matumizi ya lugha ya Kiswahili Tanzania unaobebwa na sera nyinginezo haliindwi na katiba ya nchi bali na utashi binafsi wa nani yuko ofisi gani. Kwa mfano, kuna tamko lililotolewa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete wa Tanzania kuhusu Kiswahili, likanyamazishwa bila ya kuzingatia kuwa tamko hilo la Rais Kikwete alilolitoa kuhusu Kiswahili, likanyamazishwa, lisijulikane kuwa lilitamkwa na mamlaka ya juu kabisa ya nchi.

2.3.3 Sera ya Lugha ya Ghana

Sera ya lugha ya Ghana inaonekana kuwa tafauti na ujumbe wa matumizi ya lugha unaobebwa na sera mbalimbali za Tanzania kama ilivyobainishwa katika 2.3.2. sera ya lugha ya Tanzania. Sera ya lugha ya Ghana kwa sasa inatamka kuwa Kiingereza kitatumiwa kama lugha ya kufundishia kuanzia darasa la kwanza na lugha za jamii zitakuwa masomo ya lazima katika madarasa ya juu ya sekondari (Ameyaw, 2002).

Aidha, sera ya lugha ya Ghana inatamkakuwa lugha za jamii ya Ghana zitumike kutolea baadhi ya shahada za vyuo vikuu. Kwa kufanya hivyo sera ya lugha inakuza na kuendeleza lugha za jamii. Matokeo yake ni kujiwezesha lugha hizo kufahamika na wananchi wengi wa Ghana. Tunaweza kuhitimisha kwa kusema kwamba sera yao ya lugha inatekelezeka tafauti na kile kinachosemekana kuwa ni sera ya lugha ya Tanzania ambayo baadhi ya matamko yake yamekuwa yakitoa matumaini yasiyotekelezeka. Ni kama vilekuwachezea shere wananchi wazawa wa Tanzania..

2.4 Utalii waUtafiti Uliyokwishafanyika

Wanataaluma nchini Tanzania wamekuwa wakitoa ushauri wa lugha ifaayo kufundishia. Wanataaluma hao wakiwemo Rubagumya (1996), Kiputiputi (2001) na Mlama na Matteredu (1978) wamebainisha kuwa tatizo linalosababisha wanafunzi wengi kushindwa kuzungumza au kuandika vizuri kwa lugha ya Kiingereza katika masomo yao ni mfumo mzima wa elimu ambao kimsingi unatakiwa ufanyiwe tathimini ili uimarishwe.

Mlama na Matteredu (1978) walifanya utafiti kuhusu matumizi ya lugha ya kufundishia na jinsi lugha ya kufundishia inavyoathiri elimu katika Tanzania. Katika utafiti huo walibaini kuwa uweledi wa lugha ya Kiingereza umeshuka kwa kiasi kikubwa. Kutokana na hali hiyo, matumizi ya lugha hiyo kufundishia yanawatatiza wanafunzi pamoja na walimu. Matokeo yake ni kwamba hakuna ufanisi katika kujifunza na kufundisha. Wataalamu hao walipendekeza yafuatayo: Kwanza, Kiswahili kitumike katika kufundishia elimu ngazi zote ili kutatua matatizo yanayosababishwa na matumizi ya lugha ya Kiingereza. Pili, kukuza lugha ya Kiswahili ili kuifanya iwe

lugha ya kitaalamu. Tatu, kuuimarisha ufundishaji wa lugha ya Kiingereza ili imudu mawasiliano ya kimataifa.

Utafiti uliofanywa na Mlama na Matteredu (wameshatajwa) ni tafauti na huu wetu. Wao waliangalia matumizi ya lugha ya kufundishia na jinsi lugha ya kufundishia inavyoathiri elimu katika Tanzania. Utafiti wetu unahusu mtazamo wa jamii kuhusu matumizi ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia Elimu ya juu katika vyuo vya kati. Aidha, wakati wao walijikita Utafiti huo wa Mlama na Matteredu (wameshatajwa) unatafautiana na huu wetu, utafiti wao ulijikita kuanzia ngazi ya shule za msingi mpaka ngazi ya juu ya vyuo vikuu, Wakati utafiti wetu umejikita katika ngazi ya vyuo vya elimu ya kati tu.

Criper na Dodd (1984) walifanya utafiti kuhusu lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia elimu ya sekondari. Katika utafiti huo wataalamu hao walichunguza ujuzi wa lugha ya Kiingereza walionao walimu na wanafunzi katika kufundishia na kujifunzia elimu ya sekondari nchini Tanzania. Ili kupata matokeo yakile walichokuwa wakikichunguza, wataalamu hao walitoa majaribio kwa wanafunzi elfu mbili mia nne na kumi kutoka ngazi zote za elimu.

Matokeo ya majaribio hayo yaliwafanya wataalamu hao kugunduakuwamatumizi ya lugha ya Kiingereza kufundishiana kujifunzia katika shule za sekondari siyo njia sahihi ya kutolea elimu katika ngazi hizo. uelewekakwa lugha ya Kiingereza kuko chini sana takribani katika shule zote zilizofanyiwa utafiti huo. Ni dhahiri kwamba matumizi ya Kiingereza kunafanya kujifunza kuwa kugumu. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha asilimia kumi ya wanafunzi wa kidato cha nne waliofanyiwa utafiti

walikuwa na uwezo mdogo wa kuelewa kitu chochote kilichofundishwa kwa lugha ya Kiingereza.

Pili, asilimia ishirini ya wanachuo waliokuwa katika kundi lilopimwa walikuwa na uwezo wa kusoma na kuelewa vitabu vya taaluma mbalimbali walizokuwa wanasomea. Utafiti huo umekuwa wa msaada kwa utafiti wetu kwa sababu wanachuo wa vyuo vya kati ni zao la wanafunzi wanaotokea elimu ya sekondari. Msingi mzuri ama mbovu wa lugha ya Kiingereza walio nao wanachuo wa vyuo vya kati una athari kubwa katika kujifunza na kufaulu kwao katika fani wanazosomea. Kimsingi, hujifunza lakini ufanisi haujitokezi katika mazingira ambamo wanachuo hao hawaimudu hiyo lugha ya kujifunzia ambayo ndiyo nyenzo ya kufanikishia mawasiliano katika tendo la kufundisha na kujifunza.

Msanjila (1986) alichunguza hali ya ufundishajikwa Kiswahili katika vyuo vya ualimu. Katika uchunguzi wake alibaini kwamba licha ya kuwapo kwa istilahi za kutosheleza ufundishaji wa Kiswahili, bado walimu hawazitumii katika kufundishia kwa kuwa walimu hao walipata mafunzo yao kwa lugha ya Kiingereza. Isitoshe, walimuhao hawakuwa na marejeleo ya vitabu vya Kiswahili. Kutokana na matokeo ya uchunguzi huo, alipendekeza Kiswahili kifanywe lughaya kufundishia katika shule za sekondari na vyuo vya juu ili kukiwezesha Kiswahili kuimarika na kueneza istilahi zake na kufikisha maarifa yanayotakiwa kwa jamii.

Rubagumya (1991) alichunguza utumiaji wa lugha mbili katika shule za sekondari. Kutokana na utafiti huo, mtaalamu huyo aligundua kwamba walimu walitumia lugha

zote mbili yaani Kiswahili na Kiingereza katika ufundishaji ili kuwezesha maelewano yenye manufaa baina ya walimu na wanafunzi. Hii ilitokana sera iliyomlazimishamwalimu kufundisha kwa Kiingereza ili kuwatayarisha wanafunzi kwa ajili ya mitihani inayotungwa kwa lugha hiyo. Kwa kuwa wanafunzi wanao ujuzi kidogo wa lugha ya Kiingereza, huwalazimu walimu nakukiuka matakwa ya matakwa ya sera ya kutumia lugha ya Kiingereza na badala yake hufundisha kwa lugha ya Kiswahili au kufafanua istilahi za Kiingereza kwa Kiswahili ili kuwapa hayo maarifa wanafunzi wao. Pasipo kufanya hivyo, ni wazikuwa wanafunzi hawataelewa kile wanachofundishwa.

Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa tatizo la kutomudu lugha ya Kiingereza si la wanafunzi tu, balihata baadhi ya walimu wanapata shida kufundisha kwa Kiingereza. Kutokana na utafiti huo, huendavyuo vya kati havijitengi na ukweli wa kutumia lugha mbili kwa sababu wanavyuo wao ni zao la mfumo wa elimu ya sekondari. Ipo haja kwa serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknoloji kuanzarasmi utekelezaji kwa vitendo tamko lasera ya Elimu na Mafunzo(2014) la kutumia lugha ya Kiswahili kutoa elimu na mafunzo katika ngazi zote. Kufanya hivyo kutarahisisha mchakato kwakufundisha na kujifunza kwa walimu na wanafunzi.

Mkwizu (2003) kwa upande wake alifanya utafiti juu ya matokeo ya utekelezaji wa ufundishaji wa somo la Uraia baada ya lugha ya kufundishia kubadilishwa kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza na athari zake katika shule za sekondari Tanzania.

Matokeo ya utafiti huo yameonesha kuwa katika mabadiliko ya lugha ya kufundishia na kujifunzia kutoka Kiswahili kuwa Kiingereza, kumepunguza kwa kiasi kikubwa ushiriki wa wanafunzi katika kujifunza somo hilo. Walimu waliohojiwa walibainisha kuwa ni wanafunzi wachache tu ndiyo waliokuwa wakishiriki kikamilifu katika jitihada za kweli za ufundishaji na kujifunza somo hilo. Wanafunzi wengi walikiona kitendo hicho cha kujifunza kuwa kichekesho kama cha kula mlenda kwa uma.

Mtafiti huyoanaendelea kufafanua kuwa, Kiingereza kama lugha ya kufundishia ni chanzo cha kufa kwa “demokrasia” katika juhudi za kufundisha na kujifunza darasani. Hii ina maana kuwa ujifunzaji na ufundishaji namna hiyohuyageuza mazingira ya darasani na kumfanya mwalimu na wanafunzi wachache kulitawala darasa na kuwanyima haki ya kujifunza wengi wasiojiweza. Mtafiti huyo anahitimisha utafiti wake kwa kutoa mapendekezo yafuatayo:

- i) Wale wote wanaoshiriki kwa utekelezaji wa sera kama vile walimu, wanafunzi na wazazi wahusishwe moja kwa moja katika utoaji wa maamuzi ili kufanikisha haki za demokrasia.
- ii) Wizara ya Elimu na Utamaduni inapaswa kubuni sera ya lugha ya kufundishia inayokubalika na kutekelezeka.
- iii) Serikali ifanye kampeni itakayopendelea matumizi ya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katika Shule za Sekondari Tanzania.

Utafiti wa Mkwizu (keshatajwa) umedhihirisha umuhimu wa wanafunzi kumudu lugha ya kufundishia ili kufanikisha mwendelezo wa kujifunza na kufundisha

kwaufanisi. Lugha ndiyo nyenzo ya kufanikisha mawasiliano baina ya walimu na wanafunzi.

Aidha, kwa mujibu wa UNESCO (2005), Qorro (2006) na Rajani (2006), wanafunzi wanakuwa wazuri katika kutumia maarifa (maana / dhana) endapo wataruhusiwa kutumia lugha wanayoielewa vizuri hususani ile wanayoizungumza na kuitumia kila siku katika maisha yao. Kiswahili ni lugha inayofahamika kwa watu walio wengi nchini Tanzania na kuwafanya baadhi ya watoto hasawale waishio mijini kuitumia kama lugha yao ya kwanza. Matumizi ya lugha ya Kiswahili yametamalaki kuanzia nyumbani, michezoni hadi shuleni. Matumizi yake katika kufundishia yanaweza kuwa kiungo na nyenzo muhimu katika ufundishaji na kujifunzaka wanafunzi. Watunga sera walio wengi nchini Tanzania wanapinga hoja ya kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia kwa kutoa hoja ambayo si hoja. Kwa mtazamo waowanaonakuwa ni vyema wanafunzi wajifunze katika lugha ya Kiingereza ili waweze kuimarisha uwezo wao wa kuitumia lugha hiyo, la sivyo lugha hiyo itapotea nchini Tanzania (Qorro, 2006). Kasumba kama hiyo lazima ipigwe vita kwa hali zote ili Tanzania ifikie uwezo wake yenyewe wa kujisimamisha kiuchumi kama zilivyo nchiza Finland, Sweden, Ujerumani, Japani, Uchina na India kwa kutumia lugha zao.

Rajani (2006) anaona kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia hayana maana ya kupuuza Kiingereza. Anajenga hoja kuwa wanafunzi wanapojifunza kwa lugha wanayoifahamu, hujifunza kwa ufanisi zaidi. Fauka ya hayo, lugha yao huwa nyenzo nzuri zaidi ya kumudu lugha ya pili wanayojifunza ambayo ni Kiingereza.

Mradi wa LOITASA (2005) unaoendeshwa na Chuo Kikuu cha OSLO, ulifanya utafiti kuhusu lugha za kufundishia na kujifunzia nchini Tanzania na Afrika ya Kusini. Matokeo ya utafiti yalionesha wazi kuwa matumizi ya Kiswahili katika kufundishia siyo tu yanaimarisha kujifunzanakufundisha kwa ufanisi zaidi bali pia yana manufaa kwa jamii nzima ya kitanzania. Aidha, utafiti huo ulionesha waziwazi kuwa Kiswahili nchini Tanzania ndiyo lugha inayofahamika na kutumika katika mawasiliano mapana. Kwa hiyo, mradi wa LOITASA uliipendekeza lugha ya Kiswahili itumike katika kufundishia elimu ya shule za sekondari hadi chuo kikuu. Matokeo ya utafiti wa mradi wa LOITASA yamedhihirisha kuwa mjadala ambao umekuwepo nchini Tanzania kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mfumo wa elimu hauna budi kupatiwa ufumbuzi. Wasomi na wananchi kwa jumla wanatakiwa wawe wakweli wa nafsi zao kwa manufaa yao na ya vizazi vyao kwa kukitumia Kiswahili kupeleka mbele elimu na maarifa yao kwani wahengawalisema, “Nguo ya kuazima haistiri matako.”

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Qorro na Brock-Utne (2006) nchini Tanzania kuhusu matumizi ya lugha ya Kiingereza katika kufundishia shule za sekondari, ulibaini kuwa wanafunzi wengine walimu waowana matatizo katika matumizi ya lugha ya hiyo. Wanafunzi wachache sana huweza kushiriki katika tendo la kujifunza hukuwalio wengi wakishindwa kushiriki. Kujifunzanakufundisha kunaweza kuwa na mafanikio pale tu, walimu na wanafunzi wanapomudu kutumia lugha ya kufundishia kwa sababu ufundishaji ni mawasiliano baina ya mwalimu na mwanafunzi.

Peterson alifanya utafiti (2006) kuhusu matumizi ya lugha ya Kiafrika kama lugha ya kufundishia katika ngazi ya vyuo vikuu. Mfanowake ulikuwa wa Idara ya Kiswahili katika chuo kikuu cha Dar es Salaam (tar-jama yangu). Peterson (2006) alichunguzamatumizi ya lugha ya asili ya Kiafrika kama lugha ya kufundishia katika chuo kikuu kwa kuzingatia hoja ya kuanzishwa kwa idara ya Kiswahili, mkakati unaotumiwa na idara hiyo pamoja na viwango ambavyo huwafanya walimu na wanachuo wajisikie vizuri au vibaya katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti wake yalionesha kuwa wanachuo wote waliohojiwa walikiri kuwa wanayaelewa mafunzo yaliyotolewa kwa Kiswahili kwa vizuri zaidi kuliko yale yatolewayo kwa lugha ya Kiingereza. Sababu kubwa zilizotolewa na wanachuo ni kwamba Kiswahili ni lugha ya kwanza au ya pili kwa walio wengi, ni lugha wanayoitumia nje ya darasa na ambayo hukumbana nayo katika maisha yao ya kila siku sehemu mbalimbali kama vile sokoni, nyumbani, kanisani, msikitini na hata shuleni. Wanachuo waliohojiwa walibainisha kuwa Kiingereza kinapotumika kamalugha ya kufundishiawao hujifunza kwa kiwango kidogo sana. Sababu walizozitoa ni: kutoelewa miundo ya tungo za Kiingereza, tafauti iliyopo baina ya maandishi na matamshi, baadhi ya vitabu huwa na lugha ngumu kueleweka kwa wanachuo na maneno mengi ya Kiingereza hawayaelewi kutokana na tafauti za kiutamaduni na Kifalsafa zilizopo.

Kwa upande wa walimu (Wahadhiri) waliohojiwa katika utafiti huo, walikiri kuwa Kiswahili kinafaa kuwa lugha ya kufundishia kwa sababu ni lugha inayofahamika kwa wanachuo. Kufahamika huko huwasaidia kufahamu vizuri dhana za somo pamoja na wepesi wa kujieleza kwa uhuru zaidi kwa kutumia lugha hiyo. Pia, ni

rahisi kumfahamisha mwanafunzi kwa lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na Kiingereza.

Peterson (keshatajwa) aliendelea kubainisha kwa kusema kuwakuamua kutumia Kiswahili kufundishia elimu ya juu haina maana kuwa vitabu vyote sharti vitarijuniwe kwa Kiswahili. Anahitimisha utafiti wake kwa kupendekeza kuwa Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam itumike kama mfano wa kuigwa katika kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia kozi zake zote. Utafiti mwingi umeonesha kuwa Kiswahili kina uwezo wa kujitegemea kama lugha ya kufundishia Tanzania. Utafiti huu umeusaidia kujua mtazamo wa wanafunzi na walimu (wahadhiri) wao kuhusu kutumia Kiswahili kufundishia elimu ya vyuo vikuu.

Yoradi (2013) alifanya utafiti kuhusu lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu shule za sekondari na vyuo vya ualimu. Katika utafiti huo, mtafiti alifanya majaribio ya kufundisha somo la Biolojia kwa wanafunzi wa kidato cha I, II na III kwa kutumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa mada alizozichagua kisha akatoa mtihani au majaribio ya kuwapima wanafunzi hao. Matokeo ya majaribio hayo, yalionesha kuwa wanafunzi walijifunza na kuelewawizuri zaidi na kufaulu mitihani ya somo hilo iliyotungwa kwa lugha ya Kiswahili. Hiyo ilidhihirisha maudhui ya somo la Biolojia yalieleweka vizuri zaidi kwa kufundishwa kwa lugha ya Kiswahili kuliko kwa lugha ya Kiingereza. Matokeo ya Utafiti huo yamebainisha kuwa:

- (i) Kiswahili ndiyo lugha inayoeleweka vizuri zaidi katika kufundishia nakujifunzia elimu shuleni na vyuoni.

- (ii) Wanafunzi wengi hawaelewi lugha ya Kiingereza inapotumiwakama lugha ya kufundishia. Huwafanya wanafunzi wasiweze kupata elimu ambayo wangeipata kwa manufaa ya kuliendeleza taifa.

Kutokana na utalii wa maandishi yaliyozamiwa mbizi imebainika kuwa, uamuzi wa lugha ya kufundishia, ngazi ipi ya elimu ni jambo moja na utekelezaji wake ni jambo jingine. Inahitajika mikakati thabiti na endelevu ya utekelezaji. Hivyo, sera ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia katika elimu ya juu katika Vyuo vya kati, haijitengi na ukweli huo. Linalosemwa lifanywe, likipangwa, litendeke, lakini ubinafsi, ujanjaujanja hautalinufaisha taifa. Tanzania iamue, Kiswahili kishike nafasi yake, kisomeshe, kielimishe, ili nchi na taifa lisonge mbele.

Hata hivyo Jilala (haijachapishwa) alifanya utafiti kwa kutathmini matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia ngazi zote za elimu nchini Tanzania. Lengo lilikuwa ni kufanya tathmini ya sera hiyo ili kuona kama tamko hilo ni ukombozi wa kiutamaduni ama mbio za kisiasa. Katika makala yake anajadili kuwa, matumizi ya Kiswahili ni ukombozi wa kiutamaduni ambao unadhihirisha ukombozi wa kifikra katika kutambua umuhimu wa lugha inayotambulika na jamii kama nyenzo muhimu ya kutolea na kupokea maarifa.

Tofauti na utafiti wa Jilala (haijachapishwa), utafiti huu ulichunguzwa maoni ya jamii juu ya sera ya elimu kuhusu lugha ya kufundishia ili kuona na kwa kiasi gani sera hiyo inatekelezeka. Hata hivyo, utafiti wa Jilala unatoa mwanga kuhusu sera hiyo.

2.5 Pengo la Maarifa

Kulingana utalii wa kazi tangulizi, tumebaini kuwa suala la lugha ya kufundishia katika mfumo wa elimu Tanzania, limeshughulikiwa kwa mitazamo, na kwa nyakati tofauti. Katika utafiti wa suala ili, hakuna utafiti uliyolenga kuchunguza mtazamo wa jamii juu ya Sera ya Elimu na Mafunzo kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika Vyuo vya Kati. Ingawa kuna tafiti zingine zimejadili suala la lugha ya kufundishia na sera zilizopo lakini hakuna utafiti wa kina uliofanywa kuchunguza mtazamo wa jamii juu ya Sera ya Elimu na Mafunzo kuhusu lugha ya kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati.

2.6 Mkabala wa Kinadharia

Kwa mujibu wa TUKI (2004), nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliyopangwa ili kusaidia, kueleza na kutatua au kutekeleza jambo fulani. Nadharia ni mwongozo unaoelekeza namna ya kufanya mambo kwa ufanisi na tija ili kuimarisha maisha ya mwanadamu. Kutokana na hali halisi tunasema kuwa katika maisha hakuna jambo lolote linalofanywa bila kuongozwa na nadharia. Nadharia ya nadharia, nadharia ya utafiti na nadharia ya uchambuzi (Sengo, 2009) zimetusaidia sana katika kukipendekeza Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu yenye manufaa kwa taifa.

Katika utafiti wetu, tuliongozwa na nadharia mbili ambazo ni nadharia ya kijamii na nadharia ya utekelezaji. Katika kuchunguza mtazamo wa jamii kuhusu matumizi ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati,

nadharia zilizotajwa zimetumika kukidhi madhumuni ya utafiti huo kwa kuamini kuwa nadharia hizo zitajaziana na kukamilishana kulingana na falsafa nzima ya kutumia lugha ya Kiswahilikufundishia elimu ya manufaa.

2.6.1 Nadharia ya Kijamii

Nadharia ya Kijamii iliasisiwa na Fishman (1969). Kwa mujibu wa nadharia hii, Fishman katika Giglion (1972) anaeleza kuwa tabia za wanajamii kuhusu lugha fulanihusisha matumizi ya lugha na mielekeo inayodhihirika kuhusu lugha hiyo na watumizi wa lugha hiyo. Suala amabalo linatakiwa kushughulikiwa na viongozi wa kisiasa,wasomi, viongozi wa kielimu kitaifa na kimataifani kusisitiza matumizi yalugha husika.Anaendelea kuonesha jinsi mielekeo kuhusu lughainavyotegemea muktadha wake wa kimatumizi yaani kufahamu ni nani anatumia lugha gani, kwa nani na lini katika jamii zenye wingi wa lugha. Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, tabia kuhusu lugha fulani hutegemea uwanja wa matumizi ya lugha hiyo na watumizi fulani.

Mtazamo wa kijamii wa Fishman (keshatajwa) hutumiwa kubainisha uhusiano uliopo baina ya matumizi ya lugha katika mawanda finyu (ya mtu kibinafsi) na mawanda mapana (mtu kama mwanajamii). Kibinafsi, mtu hutumia lugha kujitambua na kujitofautisha na watu wengine. Kama mwanajamii, mtu hutumia lugha kama nyenzo ya kujitambulisha kama mmoja wa wanajamii. Dhima muhimu inahusishwa na lugha fulani katika jamii pia husababisha watu kuwa na mielekeo fulani kuhusu lugha hiyo.Dhima iliyopaswa kutekelezwa na lugha fulani katika jamii hutegemea uungwaji mkono na asasi mbalimbali kama vile shule na vyuo kama

lugha ya kufundishia au lugha rasmi au lugha ya taifa. Kwa jumla dhima na matumizi tafauti ya lugha ya Kiswahili kama yanavyoelezwa katika Sera ya Elimu na Mafunzo (1995, 2014) yalitarajiwa kuungwa mkono na wakereketwa wa elimu na jamii nzima ya watanzania. Ili kufanikisha azma hiyo, serikali iwe na sera ya lugha inayojitegemea.

Kwa kuzingatia mada yetu, mtazamo wa kijamii wa Fishman (1972) ulituongozakatika utafiti huu unaohusisha uwanja wa elimu kama muktadha wa utafiti wetu.

2.6.2 Nadharia ya Utekelezaji

Nadharia ya utekelezaji iliasisiwa na Spenser (1971), mwanazuoni huyo anadai kuwa, katika matumizi ya kawaida, kugawa vipande vingi vinavyotokana na kitu kimoja kizima, ni hatari. Kwa muktadha huo lugha na jamii ni vitu viwili visivyotenganishika. Hivyo, Kiswahili hakiwezi kutenganishwa na jamii yake ya Kiafrika na badala yake, mahali pake si kuchanganywana lugha za kigeni katika juhudi za utoaji wa elimu. Kufanya hivyo ni sawa na kuingiza kiungo bandia katika mwili wa binadamu. Kiswahili kiachwe huru, kitoe elimu yenye manufaa kwa wanajamii ya Tanzania.

Maelezo ya Spenser (keshatajwa), ni mwongozo mzuri, katika utafiti huu, kwa vile, lugha na jamii havitakiwi kutenganishwa. Amali za jamii, kama vile, tamaduni, ustaarabu, mila, ujuzi na maarifa hubebwa na kurithishwa kwa lugha ya jamii (kizazi) moja kwenda nyingine (kingine). Lugha ya Kiswahili haiwezi

kutenganishwa na mfumo wa utoaji elimu katika jamii yake kwani ndiyo iliyobeba amali na utamaduni wote wa jamii ya Watanzania wanaotumia lugha ya Kiswahili kama lugha mama kwao. Kama jamii itatengwa na lugha yake ya asili iliyobeba utamaduni wa jamii hiyo, na badala yake ikatumika lugha nyingine katika kutolea elimu, basi iko hatari ya jamii hiyo kupoteza utamaduni, ujuzi wake, ustaarabu wake na amali zake na sehemu yake na kukariri tamadununi za kigeni, kuwa mtumwa wa kudumu wa kasumba na ulimbwende wa kigeni, wakujifisidi na kujihujumu wenyewe bila ya kujimaizi wala kujitambua.

Mtafiti ametumia Nadharia hii ya utekelezaji ili kuoneshea kuwa utumiaji wa lugha ya Kiingereza katika kujifunzia na kufundishia elimu katika nchi ya Tanzania ni uenezaji wa utamaduni, ustaarabu, ujuzi na maarifa ya Kiingereza na kuzika yale yote ya maana ya Watanzania. Na, kwa vile lugha hiyo ya Kiingereza ni ngeni kwa hao wanajamii wa Kitanzania, watakachokuwa wanakifanya ni kukariri na kushindwa kuelewa na kuupata vizuri ule ujuzi na maarifa ambayo wanatakiwa wayapate kwa manufaa ya nchi yao. Tanzania inahitaji kutekeleza matamko au Sera ya lugha ya Kiswahili kuweza kutumika katika kujifunzia na kufundishia katika ngazi ya Vyuo vya Kati. Sera ya lugha na Utamaduni ya Finland ni kubakia Wafini, kwa lugha na utamaduni ingawa walipata kutawaliwa na Waswidi na baadae, na Warusi, kwa zaidi ya miaka mia kidogo.

Durkheim (1971) anaunga mkono nadharia hii ya utekelezaji, kwa kuwa; ukweli waweza kuwapo pasipo kutumika, unaweza kuishi zaidi ya madhumuni yake, ama kubadili matumizi yake kwa kadri ya nyakati na vipindi. (Tafsiri yangu)

Hoja hiyo ya Dukheim (keshatajwa) ni sahihi katika mazingira ya Tanzania, ambapo Kiswahili, hakitumiki kufundishia na kujifunzia, katika ngazi zote za elimu, licha ya ukweli, kuwa ndiyo lugha inayoeleweka sana na Watanzania. Pia, lugha hii ina wazungumzaji wengi ikilinganishwa na lugha ya Kiingereza ama zote nyingine. Ukweli huo haujawahi kuwekwa katika vitendo. Sera itekelezwa, Tanzania ifikie ilipofika China au juu zaidi kwa kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu au maarifa yenye manufaa. Kwa mujibu wa wataalamu, Parsons (1949), Martindale (1960), Aberlena Wenzake (1967), Abrahmsen (1978) wanaeleza kuwa nadharia ya utekelezaji inagusia mambo yafuatayo; Uchanganuzi wa nadharia ya utekelezaji hujumuisha uweledi wa mfumo naviasilia vyake, hivyo vinahusiana ili kuweza kutumika katika mfumo husika, kila kiasilia kina mchango unaoupa uhai mfumo mzima ili uendelee kufanya kazi ama sivyo utakwamishwa iwapo viasilia vitatenganishwa, kila mfumo ni muungano wa viasilia ambavyo huunda umbo fulani lione kanalo, kila jamii ni muundo wenye vinavyohusiana na kufungamana kipekee; vinajirekebisha na kujisawazisha vyenyewe, kuendelea kuwapa kwa jamii ya watu, kunategemea mwafaka wa watu wake katika dhamira na thamani za maisha, zinazohusiana na mahitaji ya msingi ya wanajamii, ili mfumo uendelee kufanya kazi, kuna mambo ya msingi ya wanajamii yatakayoupa mfumo huo, matokeo chanya, kuwapa kwa uhusiano kati ya mawasiliano, mahitaji, uwezo na mazingira yanayoshabihika mkabala, uzoefu na mfungamano wa viasilia katika muundo wa mfumo wa jamii, utambuzi wa pamoja juu ya umuhimu wa kila kipengele kinachounda umbo fulani linalojadiliwa, utambuzi wa pamoja juu ya umuhimu wa

kila kipengele kinachounda umbo fulani linalojadiliwa, mbinu madhubuti za kusimamia tabia na mielekeo ya wanajamii.

Aidhani, nadharia hiyo ya Utekelezaji inaungwa mkono pia na Brock-Utne (2003), ambaye katika maelezo yake, anasema, lugha zinazotumika kufundishia katika madarasa ya Afrika ni lugha ambazo hazitumiwi na wanafunzi wawapo nje ya shule na wala hawaielwi kwa usahihi. Qorro (2005) anabainisha kuwa, Tanzania, kuendelea kutumia lugha ya Kiingereza kufundishia elimu ya sekondari na vyuo, ni kusababisha watu wote wanaotumia lugha hiyo kutenganishwa na jamii. Jamii ya Watanzania ina lugha zaidi ya miasita (600), inaunganishwa pamoja na Kiswahili. Wanasera hawana budi kulipa suala ili la lugha umuhimu wa kipekee.

Kimsingi, kujifunza kwa wanafunzi kuna uhusiano wa karibu sana na mfumo wa mawasiliano uliowalea na kuwakuzwa majumbani mwao. Iwapo mfumo wa elimu unatafautiana na mfumo wa mawasiliano uliyowalea wanafunzi, tutarajie matatizo katika kujifunza (Bernstein, 1971). Kwa kutumia dhana hiyo, katika jamii ya Tanzania, ambapo Kiingereza hakifahamiki sana kwa walio wengi, kwa nini nchi iendelee kutumia lugha isiyofahamika kwa wanafunzi? Haja na hoja ya msingi ni kuacha kutumia lugha ya Kiingereza kufundishia shuleni na vyuoni na badala yake kutumia lugha ya Kiswahili, inayofahamika wa wanajamii wengi nchini Tanzania.

2.7 Hitimisho

Sura hii imetalii machapisho kuhusu sera ya lugha katika kufundishia na kujifunzia. Mtafiti aliweza kutathmini sera ya lugha ya Kiswahili katika kufundishia

na kujifunzia elimu ya juu katika Vyuo vya Kati. Kilichogundulika ni kuwa, kuna uhusiano wa karibu sana kati ya lugha na jamii. Kuvitenganisha viwili hivyo, ni jambo lisilowezekana. Pia, mielelekeo ya wanajamii kuhusu lugha hutegemea dhima na matumizi ya lugha hiyo katika jamii.

SURA YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza mbinu za utafiti zilizotumika katika mchakato wa utafiti huu. Mbinu za utafiti zinajumuisha mpango wa utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, wawakilishi wa watafitia na uteuzi, mbinu za kukusanyia data, mbinu za uchambuzi wa data, maadili ya utafiti na hitimishi.

3.2 Mpango wa Utafiti

Mpango wa utafiti ni muundo wa utafiti unaoonesha jinsi utafiti ulivyofanywa katika kuchunguza tatizo la utafiti. Mpango wa utafiti hujumuisha namna data zilivyokusanywa, zana za utafiti za kukusanyia na uchambuzi wa data (Kothari, 2011), Utafiti huu umefanyika Masikanini na maktabani. Maktabani, mtafiti amehusika na usomaji wa kina wa tasnifu, majarida, vitabu na nyaraka zilizohusiana na madhumuni ya utafiti. Utafiti wa masikanini umetumiwa kukusanya data kwa njia ya usaili na hojaji kutoka kwa watafitiwa.

Mbinu ya ufafanuzi (maelezo) na takwimu (idadi) ndizo zilizotumika katika utoaji wa matokeo ya utafiti huu. Data zilikusanywa, kuhakikiwa na kuchambuliwa na hatimaye kufafanuliwa kwa kina ili ziweze kujibu maswali ya utafiti huu.

3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyika mkoa wa Mwanza, kwenye wilaya ya Nyamagana katika Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na wilaya ya Ilemela Chuo cha Maendeleo ya

Uongozi wa Elimu (ADEM). Mtafiti aliamua kufanya utafiti wake katika wilaya za Nyamagana na Ilemela kwa kuwa watafitiwa wa utafiti huu walioteuliwa, walipatikana kwa urahisi na kwa muda mfupi. Maeneo hayo yalikuwa na ukaribu wa kijiografia na eneo la makazi ya mtafiti. Pia, Vyuo vilivyoteuliwa navyo vilikuwa pia karibu. Kutokanana sababu hizo, ilikuwa rahisi wa kupata taarifa nyingi kuhusu mtazamo wa watafitiwa kuhusu tamko la sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati. Vyuo hivi vilivyoteuliwa vilikuwa kiwakilishi bora katika kukusanya data za utafiti huu.

3.4 Kundi Lengwa

Kwa mujibu wa Williman (2011) kundi lengwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika kufanyiwa utafiti yaani watu, taasisi, vitu na matukio. Kwa maneno mengine kundi lengwa ni jumla ya walengwa wote walioteuliwa kukidhi haja za utafiti. Hivyo, kundi lengwa katika utafiti huu ni wanachuo, wakufunzi wa vyuo vya CBE na ADEM, wataalamu na wadau wa elimu. Walengwa wote waliochaguliwa kushiriki kwenye utafiti huu ni miongoni mwa washikadau wa utekelezaji wa tamko la sera ya Elimu na Mafunzo(2014) na wanao uwezo wa kutoa taarifa za uhakika zilizohitajika katika utafiti huu.

3.5 Usampulishaji na Mbinu za Usampulishaji

3.5.1 Usampulishaji

Enon (1998), Spata (2003), Bryman (204) na Walliman (2004), wanaeleza kuwa usampulishaji ni mchakato wa kuchagua vitu au watu kutoka kundi lengwa ili litumike katika utafiti kama kiwaskilishi cha kundi lolote linalotafitiwa kwa kuwa sio

rahisi kutafiti kundi lengwa zima. Zipo mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa katika uteuzi wa sampuli, lakini sampuli ya utafiti huu imetumia mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu na mbinu ya uteuzi rahisi.

3.5.2 Mbinu za Usampulishaji

Uteuzi wa sampuli kwa kutumia kigezo cha madhumuni maalumu kwa kuzingatia sababu mahususi. Katika mbinu hii ya uteuzi wenye madhumuni maalumu, sampuli huteuliwa kwa kuzingatia vigezo maalumu ambavyo vitakuwa na uhusiano na maswali ya utafiti ili yaweze kujibiwa kwa urahisi na ukamilifu (Powell na Conway, 2004). Kombo na Tromp (2006) wanasema ni uteuzi ambao mtafiti kwa makusudi hulenga kuteua kundi la watu ambao anaamini kuwa ni raslimali anayoitegemea katika utafiti wake. Mbinu hii humpa mtafiti uhuru katika kuteua sampuli itakayoweza kujibu maswali ya utafiti (Neuman, 2006).

Mbinu ya uteuzi wenye madhumuni maalumu ilitumika kuteua walengwa wa utafiti huu. Kutokana na malengo ya utafiti huu, walengwa walioteuliwa ambao ni wakufunzi na wanachuo walionekana kukidhi mahitaji na kuwa na sifa ya kuteuliwa na hatimaye kufikia malengo ya utafiti huu.

Sababu nyingine ambayo ilimfanya mtafiti kutumia mbinu hii ni kwamba, mtafiti alikuwa na taarifa ya kuwepo kwa makundi yenye ujuzi, maarifa na uzoefu katika uhakiki na uchambuzi wa tamko la sera ya lugha ya kufundishia. Kwa hiyo, kwa kuzingatia ufahamu huo, mbinu hii ilitumika kuwateua wanachuo wa CBE na ADEM. Kwa kutumia kundi hili, utafiti uliweza kupata data za kutosha katika

majadiliano ya vikundi na wanachuo hao. Kwa ujumla mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu ilimsaidia mtafiti kupata sampuli ya watu wenye uzoefu, stadi na maarifa. Mbinu hii pia ilisaidia kupata data ambazo zimekuwa mhimili wa utafiti huu. Vilevile data za utafiti zilizopatikana kwa makundi hayo, zilimsaidia mtafiti kupata na kufanya majumuisho mahsusi kulingana na malengo ya utafiti.

Uteuzi wa wateule wachache hutoka kundi kubwa la watafitiwa wanaopatikana katika kundi lengwa (Yin, 1994). Utafiti huu umehusisha wawakilishi wateule 95 ambapo kulikuwa na wanachuo 60 wanaosoma kozi za stashahada katika vyuo vya CBE na ADEM. Kila chuo kilitoa wanachuo 30. Wakufunzi 10 kutoka kila chuo wanaofundisha katika vyuo hivyo na wataalamu wa elimu 15. Mgawanyowa Uteuzi huo umewasilishwa katika jedwali Na.3:1

Jedwali 3.1: Idadi ya Uteuzi wa Watafitiwa

Uteuzi wa Watafitiwa	Idadi	%	Walioshiriki	%
Wanachuo	60	63.16	60	63.16
Wakufunzi	20	21.05	20	21.05
Wataalamu na wadau wa elimu	15	15.79	15	15.79
Jumla	95	100	95	100

Chanzo: Data za utafiti (2017).

3.6 Aina za Data Zilizo Kusanywa

Kothari (2004) anasema kuna aina kuu mbili za data ambazo ni data msingi na data ya upili. Utafiti huu ulikusanya data za upili na msingi kama inavyoelezwa katika sehemu inayofuata.

3.6.1 Data za Msingi

Kwa mujibu wa Kothari (2004), data za msingi ni zile data ambazo hukusanywa kwa mara ya kwanza. Ni data halisi ambazo hazikuwahi kukusanywa na mtafiti mwingine kwa madhumuni kama haya ya utafiti huu. Katika utafiti huu, data ya msingi ilikusanywa masikanini kutoka vyuoni CBE na ADEM na mtafiti moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa ambao ndiyo wahusika wakuu wa matumizi ya lugha ya Kiswahili yanayofafanuliwa ndani ya sera ya Elimu na Mafunzo (2014).

3.6.2 Data za Upili

Data za upili ni zile data ambazo tayari zilikwishakusanywa na watafiti wengine watangulizi na kuchapishwa ama kuandikwa (Kothari, 2004). Utafiti huu ulikusanya data za upili kutokana na makala, tasnifu, wovuti, vitabu, majarida na machapishi yaliyohusiana na mada ya utafiti. Katika kufanikisha upatikanaji wa data za upili, mtafiti alitumia maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es salaama na hifadhi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

3.7 Mbinu za Utafiti

Kwa mujibu wa Kothari (2004) mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufanya utafiti. Mbinu za utafiti ziko katika makundi mawili ambayo ni mbinu za kukusanyia data na mbinu za kuchambulia data.

3.7.1 Mbinu za Kukusanya Data

Mbinu za kukusanyia data ni mbinu ambazo mtafiti alizitumia kupata data za utafiti. Utafiti huu ulitumia mbinu za aina tatu: usomajimakini wa machapishi, usaili na hojaji.

3.7.1.1 Mbinu ya Usomaji Makini wa Machapishi

Usomaji makini wa machapisho ni mbinu ya ukusanyaji wa data za upili kwa mtafiti kusoma maandishi yaliyohusiana na mada yake ya utafiti. Katika kukusanya data za utafiti huu, mtafiti alisoma kwa mzamo maandishi katika wovuti na nyaraka na akidondoa kila data iliyomfaa katika utafiti wake. Kwa kutumia mbinu hiyo, mtafiti aliweza kugundua mambo yaliyoshughulikiwa na watafiti waliomtangulia kuhusu mada ya utafiti na kukusanya data za upili za kutosha kukamilisha azma ya utafiti wake.

3.7.1.2 Usaili

Kombo na Tromp (2006) wanafafanua dhana ya usaili kuwa ni mbinu ya kukusanya data za msingi kwa kufanya mahojiano ya moja kwa moja baina ya mtafiti na mtafitiwa wake. Katika kutumia mbinu hii, mtafiti aliandaa orodha ya maswali ambayo yalimwongoza katika mahojiano aliyoyafanya na watafitiwa wake. Maswali hayoyaliendana na madhumuni mahususi ya utafiti wake. Mtafiti aliandaa mwongozo wa usaili wenye maswali tisa na kuutumia katika kukusanya data kutoka kwa wakereketwa na wataalamu wa elimu 15. Kila mtafitiwa alitakiwa kujibu maswali kutegemeana na uelewa wake na alikuwa huru kueleza kile alichokijua bila mipaka.

Kwa kutumia mbinu hii, mtafiti aliweza kukusanya data za kutosha kwa sababu ya urahisi kwa kila mtafitiwa kutoa maoni yake kwa uhuru au kuuliza pale aliposhindwa kuelewa swali. Mtafiti aliweza pia kumuuliza mtafitiwa swali la nyongeza kwa lengo la kupata maoni zaidi.

3.7.1.3 Hojaji

Hojaji kwa mujibu wa Kothari (2011) na Mligo (2012) ni mbinu ya utafiti ambayo mtafiti anaandaa maswali yake yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani. Maswali hayo yalihatiji majibu mafupi au marefu kutegemeana na taarifa iliyohitajika. Katika utafiti huu, mtafiti aliandaa mahojaji yenye maswali funge ambayo yalitoa fursa kwa watafitiwa kuchagua jibu na maswali yasiyofunge ambayo yalitoa fursa na uhuru wa kueleza walichokijua. Mtafiti aliwapa mahojaji wanachuo wa Chuo cha Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) pamoja na wakufunzi wa vyuo hivyo. Wanachuo walijaza mahojaji papo kwa papo na kuyarejesha kisha kufanya majadiliano ya pamoja na mtafiti. Wakufunzi walipewa muda wa siku tatu kujaza mahojaji na kuyarejesha kwa kuwa walikuwa na dhima nyingine za kikazi wakati zoezi la ukusanyaji data linafanyika. Mbinu hii ilitumika ili kupata taarifa nyingi zaidi kutoka kwa watafitiwa.

3.7.2 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Data za utafiti zilichambuliwa kwa kutumia mikabala ya aina mbili. Mkabala wa kiidadi na mkabala usio wa kiidadi (kimaelezo). Mkabala wa kiidadi ni mbinu ya kuchambulia data ambayo hutumia namba kurekodi taarifa na kuchambua kwa kutumia mbinu zakitakwimu. Mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya kuchambua data zilizokusanywa ulioruhusu mtafiti kueleza na kufafanua data zake kwa maelezo ya kina kwakukidhi kujibu maswali ya utafiti. Katika utafiti huu, mkabala wa kimaelezo ulitumika kwa kuwa kulikuwa na data zilizotokana na majibu ya watafitiwa zilizohitaji kutolewa maelezo. Mtafiti pia alitumia mkabala wa kiidadi kwa sababu kulikuwa na data zilizotokana na majibu yaliyofanana kutoka kwa

watafitiwa ambazozilihitaji takwimu. Data zilizopatikana ziliwasilishwa kwa kutumia maelezo na jedwali kwa njia ya asilimia.

3.8 Maadili ya Utafiti

Kazi yoyote ile huwa na kanuni na taratibu zinazopaswa kuzingatiwa katika kuitekeleza. Hali kadhalika katika kufanya utafiti huu, mtafiti alipaswa kuzingatia maadili ya utafiti ili kufanikisha kazi yake. Kabla ya kuanzazoezi la kukusanya data za utafiti huu, mtafiti alipata kibali cha kufanya utafiti masikanini kutoka Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Kibali hicho ndicho alichokitumia mtafiti kupata idhini kutoka kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza na Katibu Tawala wa Wilaya za Nyamagana na Ilemela ya kutembelea Taasisi na Ofisi za elimu ambazo zililengwa kukusanya data. Taarifa zilizopatikana kwa watafitiwa zilihifadhiwa na kutumika kwa ajili ya matokeo ya utafiti huu.

3.9 Hitimishi

Katika sura hii tumeeleza mbinu mbalimbali zilizotumika katika kupata taarifa zilizoweza kukamilika kwa utafiti huu. Vipengele vilivyoshughulikiwa katika sura hii ni pamoja na muundo wa utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, uteuzi wa wawakilishi wa utafiti, aina ya data zilizokusanywa; data za msingi na data za upili. Vipengele vingine ni mbinu za kukusanya data, usaili, hojaji na usomaji makini wa machapisho, mbinu za uchambuzi wa data na maadili ya utafiti.

SURA YA NNE

4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii imewasilisha na kuchambua data zilizohusu Kuchunguza mtazamo wa jamii juu ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 kuhusu kutumia Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika Vyuo vya Kati. Uwasilishaji na uchambuzi wa data umefanywa na kuongozwa na madhumuni mahususi na maswali ya utafiti. Data ziliwasilishwa kwa mkabala wa kitakwimu na maelezo. Hapa, tumewasilisha na kuchambua data. Kabla ya kuwasilisha data yafaa turejeele madhumuni mahususi ya utafiti huu, ambayo ni:

- i) Kubainisha tamko la sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili Kama lugha ya kufundishia na kujifunzia elimu katika Vyuo vya Kati.
- ii) Kubainisha changamoto za utekelezaji wa sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia
- iii) Kutoa mapendekezo juu ya utekelezaji juu ya sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia

Uwasilishaji na uchambuzi wa data umefanyika kwa kuzingatia lengo kuu na madhumuni mahususi ya utafiti wa mada hii pamoja na maswali ya utafiti yaliyoambatana na madhumuni hayo.

4.2 Sera ya Lugha ya Elimu na Mafunzo Kuhusu Kiswahili Kama Lugha Kufundishiana Kujifunzia

Madhumuni mahususi ya kwanza katika utafiti huu yalikuwa kubainisha tamko la sera

ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya kati. Katika kufikia dhumuni hilo, mtafiti alisoma sera ya elimu na mafunzi ili kubaini tamko kuhusu lugha ya kufundishia na kujifunzia. Mtafiti alibaini tamko la sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014 kama ifuatavyo:

Suala: Lugha ya kufundishia na kujifunzia: Umuhimu wa kuzifanya lugha ya Kiswahili na kiingereza kuwa lugha za kufundishia na kujifunzia ngazi mbalimbali uk 47.

Lengo: Kutumia lugha ya Kiswahili katika ufundishaji

Tamko: Lugha ya taifa ya Kiswahili itatumika kufundishia na kujifunzia ngazi zote za elimu nza mafunzo na serikali itaweka utaratibu wa kuwezesha matumizi ya lugha hii kuwa endelevu na yenye ufanisi katika kuwapatia walengwa elimu na mafunzo yenye tija kitaifa na kimataifa (uk. 47).

Katika nukuu hiyo ya sera, tunaona mambo matatu kwanza; suala linaelezea umuhimu wa kuzitumia lugha za Kiswahili na Kiingereza kama lugha ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi mbalimbali. Kipengele hiki kinaweza kuwachanganya wasomaji na wadau wa elimu kuwa, bado umuhimu umewekwa kwenye lugha zote mbili. Hata hivyo lengo la sera linaonesha ni kutumia lugha ya kiswahili katika ufundishaji. Sambamba na hilo tunaona tamko la sera linaweka wazi kuwa Kiswahili kitatumika kama lugha ya kufundishia ngazi zote za elimu. Hii ina maana kuwa, ufundishaji wa masomo yote katika ngazi zote za elimu utatumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya kutolea na kupokelea maarifa kwa ujumla.

Aidha, baada ya kupata data hizo, matafiti alikusanya na kuchambua data kutoka katika hojaji na usaili katika vipengele vifuatavyo:

4.2.1 Uelewa wa Wadau wa Elimu Kuhusu Tamko la Kutumia Lugha ya Kiswahili

Matokeo ya maoni ya Watafitiwa 55 ambao ni sawa na asilimia 57.89 walisema hawajawahi kusikia ama kusoma tamko la kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia vyuo vya kati. Watafitiwa 36 ambao ni sawa na asilimia 37.89 walisema wamewahi kusikia na kusoma tamko la kutumia Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu katika vyuo vya kati. Vilevile watafitiwa 04 ambao ni sawa na asilimia 4.21 walisema hawajui lolote kuhusu tamko hilo. Maoni ya watafitiwa kuhusu tamko ni kama yalivyowasilishwa kwenye Jedwali 4.1 lifuatalo:

Jedwali 4.1: Maoni ya Watafitiwa Kuhusu Tamko la Kutumia Lugha ya Kiswahili

Uteuzi wa watafitiwa	Ndiyo	%	Hapana	%	Sijui	%	Jumla	%
Wanachuo	22	23.16	34	35.79	04	4.21	60	63.16
Wakufunzi	08	8.42	12	12.63	-	-	20	21.05
Wataalamu na wadau wa elimu	06	6.32	09	9.47	-	-	15	15.79
Jumla	36	37.89	55	57.89	04	4.21	95	100

Chanzo: Data za watafiti (2017)

Jedwali 4.1 linaonesha kwamba asilimia kubwa ya watafitiwa 57.89 hawakukubali kuwa wamewahi kusoma au kusikia tamko la kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia elimu ya juu katika vyuo vya kati. Asilimia 37.89 ya watafitiwa walikubali na asilimia 4.21 ya watafitiwa hawakutoa maoni yao. Data hiyo hapo juu

inadhihirisha kwamba matamko ya sera ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu vyuo vya kati hayajawahi kuwafikia walengwa na badala yake yamebakia kwenye makabrasha ya serikali wizarani. Watanzania wengi si wasomi wakufuatilia mambo yao kwani hawana utamaduni wa kujisomea hivyo taarifa yoyote inayokuwa kwenye mfumo wa maandishi huchukua muda mrefu kuifikia jamii kubwa ya watanzania wa kawaida pasipokuwepo na uelimishaji wa kitaifa jambo husika.

Aidhani, watafitiwa 36 waliosema kuwa wamewahi kusikia ama kusoma tamko la kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati, walitakiwa kutaja mambo yaliyosisitizwa katika tamko hilo la matumizi ya Kiswahili, kufundishia na kujifunzia elimu ya Vyuo vya Kati. Matokeo ya kipengele hiki yalibainisha kuwa watafitiwa 23 sawa na asilimia 64 wanaelewa mambo yanayosisitizwa katika tamko la lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzi elimu ya vyuo vya kati. Watafitiwa 13 sawa na asilimia 36 hawajui kinachosisitizwa katika tamko hilo. Majibu ya watafitiwa ni kama yanavyoonekana katika Jedwali 4.2.

Jedwali 4.2: Majibu Yaliyotolewa na Watafitiwa Waliosema Wamesoma ama Kusikia tamko la kutumia Lugha Kiswahili

Matokeo	Majibu Yaliyotolewa				JUMLA
	A	B	C	D	
Idadi	04	06	03	23	36
Asilia	12	16	08	64	100

Chanzo: Data za utafiti (2017)

Kielelezo cha majibu yaliyotolewa

- (a) Lugha ya Kiswahili itumike kufundishia ili kukuza lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa.
- (b) Kutumika kwa lugha ya Kiswahili kutasaidia wanafunzi kuelewa kile wanachojifunza na kufaulu mitihani kuongezeka kwa sababu Kiswahili ni lugha ya umma inayoeleweka na wengi.
- (c) Lugha ya Kiswahili itumike ili kuleta uelewa zaidi kwa wanachuo juu ya yale wanayojifunza chuoni.
- (d) Kiswahili kitumike kama lugha ya kufundishia na kujifunzia ngazi zote za elimu.

Kwa mujibu wa matokeo katika jedwali 4.2 asilimia 64 ya watafitiwa wanaelewa kinachosisitizwa katika tamko la kutumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia elimu ya juu katika vyuo vya kati. Asilimia 36 ya watafitiwa hawajui mambo yanayosisitizwa katika tamko hilo. Yakichunguzwa matokeo ya watafitiwa waliowengi yanaakisi kwa kiasi fulani kauli mojawapo ya Sera ya Elimu na Mafunzo (2014) kuhusu lugha ya kufundishia isemayo, “Lugha ya Taifa Kiswahili, itatumika kufundishia na kujifunzia Elimu na Mafunzo katika ngazi zote. Serikali itaweka utaratibu wa kuwezesha matumizi ya lugha hii kuwa endelevu na yenye ufanisi katika kuwapatia walengwa elimu na mafunzo yenye tija kitaifa na kimataifa.” Aidha, matokeo hayo yanadhihirisha kwamba jamii ina uelewa kuhusu umuhimu wa matumizi ya Kiswahili elimu ya juu katika vyuo vya kati ili kujenga maarifa kwa wanafunzi.

4.2.2 Uwazi wa Sera Kuhusu Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Kufundishia na Kujifunzia.

Matokeo ya maoni ya watafitiwa yanaonesha kuwa watafitiwa 19 ambao ni asilimia 29.22 walijibu ‘ndiyo.’ Watafitiwa 40 sawa na asilimia 61.55 walijibu ‘hapana’ na watafitiwa 06 ambao ni sawa na asilimia 9.23 walisema hawajui. Maoni ya watafitiwa ni kama yanavyoonekana katika Jedwali 4.3 hapo chini.

Jedwali 4.3: Uwazi ya Sera ya Elimu Kuhusu Lugha ya Kiswahili Kufundishia na Kujifunzia.

Uteuzi wa Watafitiwa	Ndiyo	%	Hapana	%	Sijui	%	Jumla	%
Wanachuo	16	16.84	35	36.84	09	9.47	60	63.16
Wakufunzi	08	8.42	12	12.63	-	-	20	21.05
Wataalamu na wadau wa elimu	06	6.32	09	9.47	-	-	15	15.79
Jumla	30	31.58	56	58.95	09	9.47	95	100

Chanzo: Data za utafiti (2017)

Matokeo katika Jedwali hilo 4.3 yameonesha kuwa asilimia 58.95 ya watafitiwa ambao ni wengi walisema sera ya elimu haipo wazi. Watafitiwa waliosema sera hiyo ikowazi ni asilimia 31.58 na asilimia 9.47 ya watafitiwa walisema hawajui chochote. Data hiyo ni dhahiri kuwa ujumbe wa matumizi ya Kiswahili unaobebwa ndani ya sera mbalimbali juu ya Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia elimu katika vyuo vya kati hauko wazi kwa wanachuo, wakufunzi, wataalamu na wadau wa elimu. Ithibati ya hilo ni kuwa, ni miaka mitatu sasa tangu tamko litolewe, utekelezaji wake haujaanza na hakuna hatua madhubuti iliyowahi kuchukuliwa ya kuandaa mtaala wa lugha wa Kiswahili wa kozi zitolewazo na vyuo vya kati vilivyofanyiwa

utafiti ili kufanya mabadiliko ya lugha ya kufundishia kutoka Kiingereza na kuwa Kiswahili.

Aidhani, watafitiwa waliosema 'hapana' walitakiwa kutoa sababu kuhusiana na majibu yao waliyoyatoa katika 4.2.2. Sababu hizo ni kama zifuatavyo:

- i) Sera ya elimu haijaweka wazi ni lini utekelezaji wake utaanza.
- ii) Hakuna kanuni wala uteuzi wa vyombo vya kusimamia utekelezaji wake.
- iii) Sera haiko wazi kwani katika shule za sekondari na vyuo vya kati na hata vyuo vikuu bado walimu wake wanatumia lugha ya Kiingereza.
- iv) Haijaweka wazi sana dhamiri ya utekelezaji wa sera hiyo,
- v) Hakuna mjadala wa kitaifa unaowahusisha wakereketwa wa elimu kufikia maamuzi.
- vi) Nyaraka zinazohusiana na sera ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia hazijasambazwa. Wahusika wengi wa elimu hawajazipata taarifa hizo wala hawajazitafuta.

4.3 Changamoto za Utekelezaji wa Sera

Moja ya malengo mahususi yalikuwa ni kuchunguza changamoto za utekelezaji wa sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia. Utafiti huu ulibaini kuwa sera hii haijatekezwa. Watafitiwa 51 sawa na asilimia 53.68 walisema tamko la sera ya elimu na mafunzo juu ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia halitekelezeki. Watafitiwa 29 sawa na asilimia 30.53 walisema tamko la sera linatekelezeka na watafitiwa 15 sawa asilimia 15.79 walisema hawajui. Jedwali 4.4 hapa chini linawasilisha data.

Jedwali 4.4: Kutekelezeka Kwa Sera ya Elimu na Mafunzo Juu ya Kiswahili**Kama Lugha Kufundishia na Kujifunzia**

Uteuzi wa Watafitiwa	Haitekelezeki	%	Inatekelezeka	%	Sijui	%	Jumla	%
Wanachuo	29	30.52	16	16.84	15	15.79	60	63.16
Wakufunzi	13	13.68	07	7.37	-	-	20	21.05
Wataalamu wa elimu	09	9.47	06	6.31	-	-	15	15.79
Jumla	51	53.68	29	30.53	15	15.79	95	100

Chanzo: Data ya utafiti (2017)

Jedwali hilo hapo juu linaonesha kuwa asilimia 53.68 ya watafitiwa walisema sera ya Elimu juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu haitekelezeki kwa kuwa hakuna kanuni wala uteuzi wa vyombo vya kusimamia utekelezaji wa sera hiyo. Asilimia 30.53 walisema inatekelezeka kwa kuwa tayari lugha yenyewe inatumika katika nyanja mbalimbali na asilimia 15.79 walisema hawajui. Matokeo hayo yamethibitisha ukweli kuwa mpaka sasa lugha ya Kiswahili haijaanza bado kutumika katika kufundishia na kujifunzia elimu katika vyuo vya kati nchini. Hoja hii inaungwa mkono na Senkoro (2004). Pamoja na Serikali kuchochea uanzishwaji wa vyombo rasmi vya kuendeleza lugha ya Kiswahili, haijakazia matakwa na mahitaji ya utekelezaji wa sera ya Kiswahili kufundishia elimu ya viwango vyote.

Aidha, kwa kutumia hojaji wahojiwa waliulizwa kuhusu hatua ambazo zimechukuliwa na serikali katika kuhakikisha Kiswahili kinatumika kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati. Watafitiwa 46 ambao ni sawa na asilimia 70.75 walisema hakuna hatua zozote zilizowahi kuchukuliwa na serikali kuhakikisha lugha

ya Kiswahili inatumika kufundishia elimu ya vyuo vya kati. Watafitiwa 09 ambao ni asilimia 13.85 walisema kuna hatua zilizokwisha chukuliwa na serikali na watafitiwa 10 sawa na asilimia 15.38 walisema hawajui. Matokeo ya majibu ya watafitiwa ni kama yanavyoonekana katika Jedwali 4.5

Jedwali 4.5: Hatua Zilizochukuliwa na Serikali Kuhakikisha matumizi ya Kiswahili

Uteuzi wa watafitiwa	Hazipo	%	Zipo	%	Sijui	%	Jumla	%
Wanachuo	44	46.32	05	5.26	11	11.58	60	63.16
Wakufunzi	14	14.74	06	6.31	-	-	20	21.05
Wataalamuna wadau wa elimu	10	10.53	05	5.26	-	-	15	15.79
Jumla	68	71.58	16	16.84	11	11.58	95	100

Chanzo: Data za utafiti (2017)

Jedwali 4.5 linaonesha asilimia 71.58 ya watafitiwa walisema hakuna hatua zozote zilizowahi kuchukuliwa na serikali kuhakikisha lugha ya Kiswahili inatumika kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati. Asilimia 16.84 ya watafitiwa walisema kuna hatua zilizochukuliwa na serikali kuhakikisha Kiswahili kinatumika kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati. Hii ni pamoja na kutumika kwa Kiswahili kufundishia na kujifunzia stahada ya ualimu wa elimu ya awali na msingi kwa kutumia mtaala wa baraza la elimu ya ufundi (NACTE). Asilimia 15.38 walisema hawajui.

Aidhani, watafitiwa waliosema hakuna hatua zozote zilizochukuliwa walitoa sababu zifuatazo:

- i) wadau wa elimu kuhofia kuacha lugha ya kigeni itawagharimu watakapokuwa wanafanya mambo yao nje ya nchi,
- ii) lugha ya Kiswahili haijapewa kipaumbele kama ile ya Kiingereza katika ngazi zote,
- iii) hakuna mtaala unaoruhusu matumizi ya Kiswahili katika elimu ya vyuo vya kati,
- iv) bado maamuzi hayajafikiwa kutokana na matatizo ya uchumi wa dunia,
- v) Serikali iko njia panda ya kutekeleza maamuzi yake kwani hakuna hadi sasa chombo kinachosimamia utekelezaji wa sera hiyo,

Matokeo hayo yanaoneshakuwa utekelezaji wasera ya elimu juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahilikufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati,bado haijapewa kipaumbele na maofisa wa elimu walioko serikalini. Kukosekana huko kwa maamuzi madhubuti kunapingana na mapendekezo ya mfumo wa Elimu ya Tanzania 1981-2000 yanayoeleza kuwa serikali ifanye mipango thabiti ya kuziwezesha shule na vyuo vyote nchini kufundisha masomo yote kwa kutumia Kiswahili kuanzia kidato cha kwanza cha mfumo wa sasa wa elimu ya sekondari ifikapo mwezi Januari 1985 na chuo kikuu kuanzia mwaka 1992 (Tumbo,2007).

Katika kushadadia hoja hiyo, watafitiwa waliulizwa kama kuna mikakati ya utekelezaji iliyowekwa na serikali katika kufikia azima yake ya kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati. Watafitiwa 55 ambao ni sawa na asilimia 57.89 walisema hakuna mikakati ya utekelezaji iliyowekwa na serikali. Watafitiwa 33 sawa na asilimia 34.74 walikubali kuwa kuna

mikakati ya utekelezaji iliyowekwa na serikali na watafitiwa 07 ambao ni sawa na asilimia 7.37 hawakutoa maoni yoyote. Maoni ya watafitiwa kuhusu mikakati ya utekelezaji iliyowekwa na serikali katika kufikia azma yake ya kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu ya vyuo vya kati yamewasilishwa katika Jedwali 4.6.

Jedwali 4.6: Maoni ya Watafitiwa Kuhusu Mikakati ya Utekelezaji Iliyowekwa na Serikali

Uteuzi wa Watafitiwa	Hapana	%	Ndiyo	%	Sijui	%	Jumla	%
Wanachuo	33	34.74	20	21.05	07	7.37	60	63.16
Wakufunzi	12	12.63	08	08.42	-	-	20	21.05
Wataalamu wa elimu	10	10.53	05	05.26	-	-	15	15.79
Jumla	55	57.89	33	34.74	07	7.37	95	100

Chanzo: Data ya utafiti (2017)

Matokeo katika Jedwali 4.6 yanaonesha kuwa asilimia 57.89 ya watafitiwa walibainisha kuwa hakuna mikakati yoyote ya utekelezaji iliyowekwa na Serikali ili kufikia azma yake ya kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu ya vyuo vya kati. Watafitiwa wachache sawa na asilimia 34.74 ya watafitiwa walisema ipo mikakati na asilimia 7.37 walisema hawajui. Matokeo hayo yanadhihirisha kuwa Serikali haijaweka bayana lini utekelezaji wa sera hiyo utaanza. Hali hiyo inalandana na madai ya Bamgbose (keshatajwa) kuwasera za lugha nyingi katika nchi nyingi za Kiafrika ni sera za ishara ambazo zimebaki kuwa matamko au maazimio yenye nia ya kufanya mabadiliko lakini maazimio hayo hayatekelezeki. Penye nia pana njia. Kuna dalili kubwa ya kukosekana nia kwa watendaji wakuu serikalini, wizarani, na kwa wasimamizi wa sera.

Aidhani, watafitiwa waliosema ndiyo walitaja baadhi ya mikakati iliyowekwa na serikali kama ifuatavyo:

- (a) Kuwapo kwa kipindi cha televisheni ya taifa kinachosisitiza matumizi ya lugha ya kufundishia na kujifunzia kwa Kiswahili.
- (b) Kuwapo kwa kamusi imara za Kiswahili sahihi na fasaha.
- (c) Kuwapo kwa vyombo vya ukuzaji na uendelezaji wa Kiswahili safi, sahihi na fasaha.
- (d) Kuteua vyombo vya wenye lugha kudhibiti matumizi sahihi ya Kiswahili.
- (e) Kuteuliwa kwa Kiswahili fasaha kutumika katika bunge la Afrika Mashariki na la Afrika.
- (f) Kufundisha stahahada ya elimu ya shule za msingi kwa kutumia lugha ya Kiswahili kuanzia 2015/2017.
- (g) Kutumia wataalamu waliobobea na Waswahili wenyewe wanao yajua vizurimatumizi ya lugha yao ya Kiswahili.

Kwa kuzingatia sababu zilizotolewa na watafitiwa, ni dhahiri kwamba vyombo kama TATAKI, televisheni, BAKIZA, kamusi yalugha ya Kiswahili na viongozi wenye mamlaka kutoa taarifa na maamuzi yafaayo nchini. Sera iwe wazikuweka lengo la kuikuza na kuieneza lugha ya Kiswahili ili itumike kufundishia elimu nchini.

Vile vile, watafitiwa walitakiwa kutoa maoni yao iwapo kuna shida kama lugha ya Kiswahili ikitumika katika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati. Matokeo yalionesha kuwa watafitiwa 38 sawa na asilimia 40 walisema kuna shida kama lugha ya Kiswahili itatumika katika kufundishia na kujifunzia elimu ya

vyuo vya kati. Watafitiwa 54 sawa na asilimia 56.84 walisema Kiswahili kinakidhi dhima ya kutumika katika mfumo wa elimu na watafitiwa 03 sawa na asilimia 03.16 walisema hawakuwa na maoni yoyote.

Jedwali 4.7: Maoni ya Watafitiwa Juu ya Kutumia Lugha Kiswahili katika Kufundishia na Kujifunzia

Uteuzi wa Watafitiwa	Hapana	%	Ndiyo	%	Sijui	%	Jumla	%
Wanachuo	30	31.58	27	28.42	03	03.16	60	63.16
Wakufunzi	15	15.79	05	05.26	-	-	20	21.05
Wataalamu na wadau wa elimu	09	9.47	06	06.32	-	-	15	15.79
Jumla	54	56.84	38	40.00	03	03.16	95	100

Chanzo: Data za utafiti (2017)

Jedwali Na.4.7 linaonesha kuwa asilimia 56.84 ya watafitiwa walisema kuna shida kama lugha ya Kiswahili itatumika katika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu ya vyuo vya kati. Asilimia 40 ya watafitiwa walisema hakuna shida yoyote itakayokuwepo kama lugha ya Kiswahili ikitumika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati na asilimia 03.16 ya watafitiwa hawakuwa na maoni yoyote.

Aidhani, watafitiwa waliosemakuwa Kiswahili hakikidhi kutumika kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati walitoa sababu kama zinavyobainishwa hapa chini:

- i) itaathiri wanafunzi na wakufunzi wasipende kutumia kabisa lugha ya Kiingereza.

- ii) wanafunzi watakosa soko la dunia kwani Kiingereza ni lugha ya kimataifa hivyo kukosa nafasi ya kufundisha mataifa mengine.
- iii) itafinya uwanja katika ulimwengu wa ajira, ushindani na utumiaji wa Kiingereza.

Matokeo hayo yanaonesha kuwa baadhi ya watafitiwa wanahofu ya kutumika kwa lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati. Kimsingi, mabadiliko yoyote, yawe ya kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kiteknolojia huibua hofu za msingi na zisizo za msingi kwa baadhi ya wanajamii kwa sababu ya mazoea na imani iliyojengeka kutokana na mfumo uliowalea na kuwakuza. Hivyo mabadiliko yanaogopwa. Uthibitishi wa mabadiliko kutokidhi matarajio ni baadhi ya watafitiwa kuona kuwa lugha ya Kiswahili haiwezi kuendana na utunduizi na kufinya uwanja katika ushindani wa ajira na utumiaji wa Kiingereza.

Aidha, watafitiwa waliosema Kiswahili kitumike kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati walikuwa na maoni yafuatayo:

- i) Italeta ufanisi katika kujifunza,
- ii) Itawasaidia wanafunzi kuelewa vyema kinachofundishwa,
- iii) Itakua, itaenea na kutambulikana na mataifa mengine.

Kwa kuzingatia Watafitiwa walio wengi (56.84%) ambao wameonesha kuwa Kiswahili kinaweza kutumika kufundishia nakujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati bila ya matatizo. Mtafiti ameshawishika kukubaliana na hoja hiyo ya watafitiwa wengi kwa kuzingatia uhalisi wa kile kinachotokea katika mazingira ya ndani na nje na vyuo ambapo lugha zote mbili Kiingereza na Kiswahili hutumika katika

kufanikisha mawasiliano baina ya wanaofundisha, wanaojifunza na wanajamii kwa ujumla. Kwa hiyo, zinahitajika hatua za makusudi zitakazoweza lugha ya Kiswahili kuchukua nafasi yake ya kutumika kutolea elimu ya juu.

Pamoja na data hizo na maelezo ya watafitiwa kuhusu utekelezaji wa sera lakini bado wahojiwa walidokeza kuwa lugha ya Kiswahili imekuwa ikitumika katika mijadala ya kitaaluma hata kama lugha ya Kiingereza inatumika kufundishia. Watafitiwa 65 ambao ni sawa na asilimia 68.42 hutumia lugha ya Kiswahili katika kufanya majadiliano ya mada anuai. Watafitiwa 30 ambao ni sawa na asilimia 31.58 hutumia lugha ya Kiingereza wakati wa majadiliano ya baadhi ya madawanazofundishwa chuoni. Muhtasari wa matokeo ya majibu ya watafitiwa ni kama yanavyoonekana katika Jedwali 4.8.

Jedwali 4.8: Matumizi ya lugha ya Kiswahili ama Kiingereza katika Mijadala ya

Mada Wanazojifunza

Uteuzi wa watafitiwa	Kiswahili	Asilimia	Kiingereza	Asilimia	Jumla	Asilimia
Wanachuo	43	45.26	17	17.89	60	63.16
Wakufunzi	13	13.68	07	7.37	20	21.05
Wataalam na Wadau wa elimu	09	09.47	06	06.32	15	15.79
Jumla	65	68.42	30	31.58	95	100

Chanzo: Data za utafiti (2017)

Katika Jedwali la 4.8 hapo juu kumeoneshwa kuwa asilimia 68.42 ya watafitiwa wanatumia lugha ya Kiswahili katika kufanya majadiliano juu ya mada za kitaaluma na kijamii. Asilimia 31.58 ya watafitiwa wanatumia lugha ya Kiingereza wanapojadiliana.

Kutokana na matokeo hayo, watafitiwa wameonesha kuwawatafitiwa walio wengi hufanya majadiliano ya masomo na mada nyingine kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hii inadhihirisha kuwa Kiswahili ndio lugha inayoeleweka na kutumiwa na wanachuo, walimu na jamii kubwa ya Watanzania katika mazingira ndani na nje ya mazingira ya shule na vyuo. Matokeo hayo ni uthibitishi tosha kuwa lugha ya Kiswahili ikipewa fursa rasmi ina uwezo wa kufanikisha ujifunzaji wa masomo pamoja na mawasiliano katika nyanja zote katika vyuo vya kati.

4.4 Mapendekezo

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa ni kutoa mapendekezo juu ya sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia. Matokeo yalikuwa katika pande mbili; kwanza wahojiwa waliulizwa juu ya mapendekezo yao juu ya matumizi ya Kiingereza na Kiswahili na Pia maoni na mapendekezo yao. Sehemu zifuatazo zinawasilisha data na matokeo ya utafiti huu.

4.4.1 Mchango wa Lugha ya Kiingereza katika Kufundishia na Kujifunzia

Mtafiti, aliwataka watafitiwa kueleza mchango wa lugha inayotumika ya Kiingereza katika kujifunzia au kufundishia mada za masomo kwa kuhusisha kufaulu kwao na ubora wa mafunzo yanayotolewa. Watafitiwa 30 sawa na asilimia 31.58 walikubali kuwa lugha inayotumika inamchango katika kufaulu na ubora wa mafunzo yanayotolewa. Watafitiwa 57 sawa na asilimia 60 hawakukubaliana na hoja hiyo. Watafitiwa 8 sawa na asilimia 8.42 hawakutoa maoni yoyote. Muhtasari wa majibu ya watafitiwa ni kama unavyoonekana katika Jedwali 4.9.

Jedwali 4.9: Maoni ya watafitiwa kuhusu Mchango wa lugha ya Kiingereza katika Kufundishia na Kujifunzia

Uteuzi wa Watafitiwa	Hapana	%	Ndiyo	%	Sijui	%	Jumla	%
Wanachuo	33	34.74	19	20.00	08	08.42	60	63.16
Wakufunzi	13	13.68	07	07.37	-	-	20	21.05
Wataalamu na wadau wa Elimu	11	11.59	04	04.21	-	-	15	15.79
Jumla	57	60	30	31.58	08	08.42	95	100

Chanzo: data ya utafiti (2017)

Katika jedwali la Masikanini 4.9, matokeo yanaonesha kuwawatafitiwa wengi asilimia 60 ya watafitiwa wote hawakubaliani na mchango wa lugha ya Kiingereza inayotumiwa katika kujifunzia na kufunziwa mada za masomo kuwa inahusiana na kufaulu kwao na ubora wa mafunzo yanayotolewa chuoni. Asilimia 31.58 ya watafitiwa walisema lugha inayoyumika ina mchango kwa kufaulu na ubora wa mafunzo yanayotolewa chuoni. Asilimia 8.42 hawakuwa na maoni yoyote kuhusu hoja hiyo. Matokeo haya yalitafasiriwa kuwa lugha yoyote inayotumika katika mchakato mwendelezo wa ufundishaji na ujifunzaji ina mchango wa kufanikisha au kukwamisha ufanisi wa ubora wa mafunzo yanayotolewa.

Aidha, watafitiwa waliokubali kuhusu mchango wa lugha ya Kiingereza inayotumika katika kujifunzia au kufunziwa mada za masomo kwa kuhusisha kufaulu kwao na ubora wa mafunzo yanayotolewawalikuwa na maoni yafuatayo:

- i) Inasaidia wanajamii kujiamini, kuinua kiwango cha kufaulu na utendaji wa kila mwanachuo
- ii) Lugha ndicho chombo pekee kinacho msaidia mtu kupokea au kutoa taarifa kwa kutumia dhana za jamii

- iii) Lugha inayotumika inawafanya wanajamii waelewe zaidi na kupata umahiri, uweledi na ufanisi maishani.
- iv) Kiingereza kina mchango mkubwa katika ubora wa mafunzo yanayotolewa.
- v) Lugha ya Kiingereza inamuweka sawa mwanafunzi katika kujiamini na kutenda mambo kwa viwango vya juu
- vi) Kiingereza kwa sasa ni bidhaa ya kupata ajira katika makampuni ya kigeni na hata nje ya nchi.

Kutokana na sababu zilizotolewa na watafitiwa hapo juu, mtafiti anashawishika kusema kuwa lugha ya Kiingereza bado inaonekana kuwa na nafasi finyu ya kutumika katika ujifunzaji na ufundishaj unaoleta kufaulu zaidi na ubora wa mafunzo yanyotolewa. Hata hivyo, jitihada za makusudi zinahitajika katika kuimairisha na kujenga misingi thabiti ya lugha ya Kiingereza ili iweze kuenea na kufahamika kwa walio wengi.

Kwa upande wa watafitiwa waliosema ‘hapana’ walitoa maoni yafuatayo kuhusiana na mchango wa lugha ya Kiingereza inayotumika katika kujifunza au funzwa mada za masomo kwa kuhusisha kufaulu na ubora wa mafunzo yanayotolewa kwa sasa:

- i) Baadhi ya wanafunzi na walimu hawana umilisi wa kutosha wa lugha ya Kiingereza na hivyo huathiri ubora wa mafunzo yanayotolewa.
- ii) Lugha inayotumika kufundishia na kujifunzia haifahamiki vizuri kwa walimu na wanafunzi.

- iii) Wanafunzi na walimu hutumia muda mwingi katika kujenga dhana ya jambo linalofunzwa kwani hulazimika kufikiri kwa Kiswahili na kuandika kwa lugha ya Kiingereza
- iv) Lugha ya Kiingereza husababisha wanachuo wengi kushindwa katika mitihani yao kwa kutoimudu lugha hiyo,
- v) Haina mchango mkubwa katika kufaulu na ubora wa mafunzo kwani ni lugha ngeni kwa wanafunzi na walimu.

Matokeo hayo yanadhihirisha kuwa matumizi ya lugha ya ngeni yanaathiri viwango vya ufaulu kwa wahitimu au wanachuo pamoja na ubora wa mafunzo yanayotolewa. Hali hii inafanana na ile inayowapata wanafunzi wa shule za sekondari kama inavyoelezwa na Tumbo (2007) kuwa tatizo lingine kubwa ambalo limesababisha kushuka kwa viwango vya elimu ni kudorora kwa Kiingereza. Mpemba (2007) na Swilla (2009) wanadai kuwa walimu wengi wa Tanzania hawana umilisi wa kutosha wa lugha ya Kiingereza. Udhaifu huu katika lugha ya Kiingereza husababisha walimu kupata ugumu katika kufundisha masomo ya elimu ya sekondari kwa ufanisi hivyo kusababisha wanafunzi kutopata maarifa ya kutosha yaliyokusudiwa kwa ajili yao. Ukweli wa wataalamu hao unadhihirisha hali halisi ya kile kinachofanyika katika madarasa ya shule na vyo ambapo baadhi ya walimu hutumia Kiingereza na Kiswahili kufundishia ili wanafunzi wao waelewe. Kwa muktadha huo tunaona kuwa lugha ya Kiswahili inadai nafasi yake ya kutumika ili kuwezesha mawasiliano chanya katika kufanikisha tendo la kujifunza. Hivyo ipo haja ya lugha ya Kiswahili kuhalalishwa kutumika katika kufundishia na kutolea elimu nchini.

4.4.2 Manufaa ya Kutumia Lugha ya Kiswahili katika Kufundishia na Kujifunzia

Kwa kutumia hojaji na usaili, watafitiwa waliulizwa kuhusu manufaa ya lugha ya Kiswahili kutumika kama lugha ya kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati. Watafitiwa 77 sawa na asilimia 70.53 walikubali kuna manufaa ya lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati. Watafitiwa 16 sawa na asilimia 16.84 walijibu hawakuwafiki na watafitiwa 12 ambao ni sawa na asilimia 12.63 hawakujibu chochote. Maoni ya watafitiwa kuhusu manufaa ya kutumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati yanawasilishwa katika jedwali 4.10, lifuatalo:

Jedwali 4.10: Maoni ya Watafitiwa Kuhusu Manufaa ya Kutumia Lugha ya Kiswahili katika Kufundishia na Kujifunzia

Uteuzi wa watafitiwa	Ndiyo	%	Hapana	%	Sijui	%	Jumla	%
Wanachuo	44	46.32	09	9.47	07	07.37	60	63.16
Wakufunzi	15	15.79	04	4.21	01	01.05	20	21.05
Wataalamu na wadau wa elimu	08	08.42	03	3.16	04	04.21	15	15.79
Jumla	67	70.53	16	16.84	12	12.63	95	100

Chanzo: Data ya utafiti (2017)

Matokeo katika Jedwali 4.10 hapo juu yanaonesha kuwa watafitiwa wengi ambao ni asilimia 70.53 wamekubaliana na wazo la kutumiwa lugha ya Kiswahili kujifunzia na kufundishia elimu ya vyuo vya kati. Matokeo hayo yanashabihiana na hoja ya Peterson (keshatajwa), kuwawanafunzi wana mawazo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili na kwamba wanaelewa vizuri wanapofundishwa kwa lugha hiyo. Hii ni

kwa sababu Kiswahili ni lugha wanayoitumia nje ya darasa na popote kama sehemu ya maisha yao ya kila siku. Wanafunzi wanapoitumia katika ujifunzaji hupata maarifa na kujenga umahiri katika fani wanazosomea.

Aidha, watafitiwa waliokubaliana na wazo la kutumiwa lugha ya Kiswahili kujifunzia na kufundishia elimu ya vyuo vya katiwalikuwa na hoja zifuatazo:

- i) Itasaidia wanachuo kuelewa zaidi maudhui wanayofunzwa.
- ii) Itachochea kuongezeka kwaufaulu.
- iii) Itarahisisha kuelewa masomo na kujijengea umahiri.
- iv) Itasaidia walimu na wanafunzi kuwasiliana kwa urahisi katika muendelezo wa kufundisha na kujifunza
- v) Itasaidia kutunza, kuhifadhi asili yetu, utaiifa wetu na amali tulizo nazo.

Kwa kuzingatia matokeo hayo, watafitiwa walio wengi wanaafiki kuwa Kiswahili kikitumika kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati kitakuwa na mchango mkubwa katika kurahisisha mawasiliano baina ya walimu na wanafunzi na itawafanya wanafunzi kujenga umahiri na weledi wa fani wanazojifunza vyuoni. Matumizi ya lugha ya Kiswahili yatawawezesha wanachuo kujinasibisha na kujifungamanisha na jamii yao ya Kitanzania. Hoja hii inaungwa mkonona Msanjila na wenzake (2011) kwamba matumizi ya lugha sahihi katika kufundishia masomo katika mfumo wa elimu ni zaidi ya kuwasaidia wanaojifunza kwa sababu huendeleza vipaji vyao na kubwa zaidi lugha hiyo huendelezwa ili kukabili mabadiliko ya ulimbe na utunduizi.

Kutotumia lugha ya Kiswahili kufundishia elimu ya Tanzania hakuwasaidii wanafunzi kufikia malengo yao. Watafitiwa ambao hawakukubaliana na wazo la Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati, walikuwa na hoja zifuatazo;

- i) Haitawapa wanafunzi fursa ya kuchangamana na mataifa mengine kwa vile hawajui lugha ya Kiingereza,
- ii) Itadumaza Watanzania kutumia lugha ngeni katika kujifunza na mawasiliano.
- iii) Haijitoshelezi kimsamiati

Matokeo hayo yanadhihirisha kuwa baadhi ya wakereketwa wa elimu wakiwemo wanachuo, wakufunzi (wahadhiri), wataalamu na wasomi wanaona kuwa Kiswahili hakifai kutumika kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati. Hii ni uthibitishi kuwa bado wana kasumba ya kutawaliwa na wakoloni na wanaamini usomi, ustaarabu na kuelimika kunaambatana na utumizi wa lugha ya Kiingereza. Mtazamo huona tofautianana Rubanza (keshatajwa), kwamba wanafunzi wa Tanzania hupoteza ujuzi wa lugha ya Kiingereza mara tu wanapohitimu elimu yao kwa sababu jamii inayowazunguka haitumii lugha hiyo.

4.4.3 Athari ya Kutotekelezwa kwa Matamko ya Sera ya Elimu na Mafunzo juu ya Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Kufundishia Vyuo vya Kati

Kwa kutumia mbinu ya hojaji na usaili, mtafiti aliwataka watafitiwa kutoa maoni yao kama kuna athari zitokanazo na kutotekelezwa kwa tamko la matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu ya Vyuo vya Kati. Watafitiwa 57 sawa na asilmia 60 walifiki kuwa kutokutekelezwa kwa matamko ya Sera ya

matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati. Watafitiwa 33 sawa na asilimia 34.74 hawakukubaliana na hoja hiyo na watafitiwa 5 sawa na asilimia 5.26 hawakujibu chochote. Matokeo ya watafitiwani kama yanavyooneshwa katika Jedwali 4.12:

Jedwali 4.11: Maoni ya Watafitiwa Kuhusu Athari ya Kutotekelezwa kwa Tamko la Matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika Kufundishia na Kujifunzia katika Vyuo vya Kati

Uteuzi wa watafitiwa	Ndiyo	%	Hapana	%	Sijui	%	Jumla	%
Wanachuo	38	40.00	18	18.95	04	04.21	60	63.16
Wakufunzi	15	15.79	05	05.26	-	-	20	21.05
Wataalamu wa elimu	04	04.21	10	10.53	01	01.05	15	15.79
Jumla	57	60.00	33	34.74	05	05.26	95	100

Chanzo: Data ya utafiti (2017)

Matokeo hayo yanatanabaisha kuendelea kushamiri kwa matumizi ya uwili wa lugha katika ufundishaji na ujifunzaji wa elimu ya vyuo vya kati. Hali hiyo inasababisha wanafunzi wakose umahiri na uweledi katika kumudu na kutumia kwa ufasaha lugha ya Kiingereza au Kiswahili kwa viwango stahiki.

Aidha, kipengele cha pili cha hojaji au mwongozo wa usaili kiliwataka watafitiwa waliokubali kuwapo kwa athari zitokanazo na kutotekelezwa kwa tamko la matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati.

Majibu ya watafitiwa yalikuwa ni haya yafuatayo:

- i) Kudumaza maendeleo ya ukuzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Tanzania

- ii) Kiingereza kuendelea kutumika na kuonekana kuwa ndiyo lugha ya usomi na ustaarabu wa Watanzania.
- iii) Kujengeka kwa mielekeo hasi miongoni mwa wanajamii kuhusu lugha ya Kiswahili inayodunisha na kukwamisha uendelezaji na utoaji wa fursa ya kutumika kwa lugha hiyo katika ufundishaji na ujifunzaji wa elimu ya juu.
- iv) Uwili lugha kuendelea kutumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa elimu ya vyuo vya kati.
- v) Baadhi ya wahitimu wa elimu ya vyuo vya kati kutokuwa na uweledi wa kutumia lugha ya Kiingereza au Kiswahili kwa ufasaha.
- vi) Kutofikiwa kwa muafaka wa mjadala unaoendelea juu ya lugha ipi itumike katika ujifunzaji na ufundishaji wa elimu ya juu.

Matokeo hayo yanadhihirisha kuwa jitihada kubwa za makusudi zinahitajika kubadili mtazamo wa jamii ili kupata mustakabali wa lugha ifaayo katika utoaji wa elimu bora kwa viwango tafauti vya elimu. Akilizungumzia suala kama hili, Halliday (1973) anasema, lugha ya mawasiliano katika jamii ndiyo ifaayo kuwa lugha ya kufundishia kwa kuwa ndiyo lugha ambayo wanafunzi wanaifahamu vizuri. Lugha ya mawasiliano katika jamii inapopewa dhima ya kufundishia hukua na kuweza kueleza nyanja mbalimbali za maarifa. Sifa hizo zinabebwa na lugha ya Kiswahilina kwa hali hiyo inastahili kupewa kipaumbele cha kutumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa elimu ya vyuo vya kati na vyuo vikuu. Fauka ya hayo, kwa sababu thamani na majukumu yanayotekelezwa na lugha yoyote katika jamii ya wingi lugha huathiri mielekeo na tabia za wanajamii katika kujifunza, kuithamini na kuitumia lugha hiyo.

4.4.4 Changamoto za Utekelezaji Tamko la Sera ya Elimu Juu ya Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Kufundishia na Kujifunzia Vyuo vya Kati

Watafitiwa walitakiwa kubainisha changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati. Watafitiwa walitoa majibu yafuatayo:

- i) Kutokuundwa kwa vyombo vya kusimamia utekelezaji wa sera ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu,
- ii) Uchumi ni kikwazo katika kufanya mabadiliko ya lugha ya kufundishia kutoka Kiingereza kuwa Kiswahili,
- iii) Katiba ya nchi kutokutamka waziwazi kuhusu matumizi ya Kiswahili katika kujifunzia na kufundishia elimu ya juu ya vyuo vya kati.
- iv) Utayari wa wanafunzi na walimu watakaotumia lugha hiyo katika kujifunza na kufundisha,
- v) Mielekeo ya wakereketwa wa elimu kuhusu lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia na uhaba wa wataalamu wa kutarijamu vitabu kutoka lugha ya Kiingereza kuwa Kiswahili kujifunzia elimu ya juu

Kutokana na matokeo hayo ni dhahiri kuwa kuna changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati. Hata hivyo, lengo la kuzalisha wataalamu shuleni na vyuoni ni kuwahudumia Watanzania ambao ni wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa mantiki hiyo kuna haja ya kuangalia uwezekano wa kuondoa changamoto hizo ili kuwezesha wanachuo kupata fursa ya kujifunza taaluma zao

mbalimbali kwa kutumia lugha ya Kiswahili ambayo wanategemea kuitumia katika utoaji wa huduma kwa wananchi wa taifa lao.

Baada ya kupata maoni ya watafitiwa kuhusu utekelezaji wa sera, utafiti huu unakubaliana na maoni yaliyotolewa na Jilala (haijachapishwa) kuwa utekelezaji wa sera ya elimu inayosema Kiswahili kitumike kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu. Jilala anapendekeza mambo mbalimbali ili kutekeleza sera ya elimu kuhusu lugha ya kufundishia kama ifuatavyo:

4.4.4.1 Kwa Serikali

Serikali inatakiwa kutoa msimamo thabiti katika kuiweka wazi sera hiyo iwe wazi na bayana. Tukitazama nchi na mataifa makubwa ambayo yamefikia mendeleo ya kweli yalijikita katika kuheshimu elimu na kutumia lugha yao ya jamii kutolea na kupokelea maarifa. Ikumbukwe kwamba elimu ndiyo mkombozi wa jamii na ni daraja la maendeleo ya jamii yoyote. Kwa hiyo, endapo elimu itakuwa ina legalega basi tusitegemee kuuondoa umaskini katika jamii zetu.

4.4.4.2 Kutoa Elimu kwa Wadau

Serikali ishirikiane na wataalamu wa Kiswahili na taasisi za Kiswahili kutoa elimu kwa wadau wa elimu, kutoa mafunzo na kuendesha warsha mbalimbali kwa walimu wa ngazi zote kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia. Elimu hii itasaidia kuondoa dhana na kasumba zilizopo miongoni mwa baadhi ya wadau kuwa lugha ya Kiswahili haijitoshelezi katika misamiati na hivyo haifai kutumika kama lugha ya kufundishia. Aidha, elimu itasaidia kuwaandaa na kuwapa mafunzo wadau wa elimu ambao ndio watakaotumia lugha ya Kiswahili.

4.4.4.3 Kuongeza Bajeti ya Elimu

Mchakato wa kufanya mabadiliko ya matumizi ya lugha ya kufundishia si zoezi dogo. Ni zoezi ambalo linahitaji maandalizi makubwa ndani ya serikali hii nipamoja na kuhakikisha kuna bajeti ya kutosha kutekeleza sera hiyo. Kuongeza bajeti ya elimu kutasaidia kuendesha warsha, mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu, kuandaa kamusi na kuboresha na kuunda istilahi za maarifa mbalimbali, kutafsiri vitabu vya kiada na vya rejea vitakavyotumika katika kufundishia na kujifunzia.

4.4.4.4 Kuanzisha Shule za Kiswahili

Serikali inahitaji kuteua shule maalumu za Kiswahili kuanzia ngazi ya awali mpaka vyuo vikuu. Kwa kufanya hivi, tutaweza kuwa na shule za mfano ambazo zitasoma kwa kutumia lugha ya Kiswahili masomo yote kuanzia ngazi ya chekechea hadi chuo kikuu huku lugha zingine za kimatifa zikifundishwa kama somo. Kufanikiwa kwa shule hizi kutaondoa fikra, hofu na kasumba iliyojengeka akilini mwa wanachi tangu awali kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika elimu. Pia itatoa fursa kwa jamii na serikali kutathimini ubora wa matokeo ya wahitimu katika mfumo huo kwa kulinganisha na mfumo uliopo.

4.4.4.5 Nafasi za Lugha Zingine

Serikali inatakiwa kuhaikisha kwamba lugha ya Kiswahili inakuwa lugha ya kufundishia na kutumika katika mawasiliano yote rasmi bila ukakasi. Sambamba na hilo, ili tusiachane na dunia, serikali inatakiwa kuhakikisha kwamba lugha kuu duniani kama vile Kiingereza, Kijerumani, Kichina, Kifaransa nk zinafundishwa na walimu mahiri ambao wamepata mafunzo, mbinu na kanuni za ufundishaji wa lugha

ya pili na kundelea. Mkakati huu utasaidia kuzijua lugha zingine duniani na kuweza kuzitumia katika mawasiliano mahususi na hili litatufanya tusiachane na ulimwengu na jamii zingine.

4.4.4.6 Kwa Jamii

Mapendekezo kwa jamii ambao ndiyo wadau wa elimu ni kwamba jamii inahitaji kupewa elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa lugha na utamaduni wa jamii. Makala haya yalibaini kuwa, wanajamii wengi hasa wazazi wanaamini kwamba Kiswahili si lugha ya kimataifa kwa hiyo kuwekeza katika elimu ambayo imejikita katika Kiswahili ni kuwapoteza watoto wao na kuwafanya wawe nje ya ulimwengu. Dhana hii ni dhana potofu japo ina mashiko. Kitu cha msingi ni kutoa elimu ili kasumba hii itoke katika fikra za wanajamii na waipokee lugha ya Kiswahili kwa mtazamo chanya. Waelewe sababu za kutumia Kiswahili na waelezwe nafasi ya Kiingereza katika mfumo huu. Waelewe lugha zingine zitakuwa na nafasi gani katika jamii yetu, Wawekwe wazi kuhusu mikakati ya lugha zingine na matumizi ya lugha hizo katika jamii.

4.4.4.7 Kupandikiza Fikra ya Mapinduzi ya Lugha

Jamii ipewe elimu kuwa mpaka sasa tupo katika ukoloni wa kiutamaduni ambao unaathiri lugha na utaiifa. Kwa hiyo, matumizi ya Kiswahili ni fikra za mapinduzi ya lugha kujikomboa katika ukoloni lugha na kuwa huru kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa. Aidha, jamii Jamii ipewe elimu kuwa.matumizi ya lugha ni utambulisho wa utaiifa na utamaduni wa jamii na zaidi ni fikra ya mapinduzi.

4.5 Hitimishi

Sura hii imewasilisha na kufafanua matokeo ya utafitiunaohusu mtazamo wa jamii juu ya sera ya elimu na mafunzo 2014 kuhusu kutumia Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati.

Uwasilishaji na uchambuzi wa data umefanyika kwa kuzingatia madhumuni mahsusi ya utafiti na umeongozwa na mkabala usio wa kiidadi na wa kiidadi. Utafiti umebaini uwepo wa matamko yanayohusu kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati, sera ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati haiko wazi kwa wadau wa elimu na umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati. Vile vile utafiti umebaini matatizo ya utekelezaji wa sera ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu katika vyuo vya kati na athari za matumizi ya lugha ngeni ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia elimu katika vyuo vya kati.

SURA YA TANO

5.0 MUHTASARI, HITIMISHI NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii inahitimisha utafiti unaohusu kuchunguza mtazamo wa jamii juu ya sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka (2014) kuhusu matumizi ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Kati. Sura hii imegawanyika katika sehemu sita. Sehemu ya kwanza inaelezea muhtasari wa utafiti. Sehemu ya pili inaelezea matokeo ya utafiti. Sehemu ya tatu inaelezea hitimishi la utafiti. Sehemu ya nne inaelezea manufaa ya utafiti. Sehemu ya tano inaelezea mapendekezo ya utafiti. Sehemu ya sita inaelezea maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa utafiti zaidi na sehemu ya mwisho ni hitimishi la sura.

5.2 Muhtasari Kuhusu Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza mtazamo wa jamii juu ya sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka (2014) kuhusu matumizi ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Kati. Utafiti huu umefanyika wilaya za Nyamagana katika Chuo Cha Elimu ya Biashara (CBE) na wilaya ya Ilemela katika Chuo Cha Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) mkoa wa Mwanza. Ili kufanikisha lengo kuu, utafiti ulikuwa na madhumuni mahsusi matatu ambayo ni; kubainisha tamko la sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia elimu katika vyuo vya kati, kubainisha changamoto za utekelezaji wa sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia na kutoa mapendekezo juu ya utekelezaji juu ya sera ya

elimu kuhusu matumzi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia. Utafiti huu uliwashirikisha watafitiwa 95 waliotumika kama wawakilishi wa utafiti huu. Data za utafiti huuzilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili hojaji na usomaji makini wa machapishi. Uwasilishaji na uchambuzi wa data umefanyika kwa kuzingatia madhumuni mahsusi ya utafiti na ulitumia mkabala wa kiidadi na usio wa kiidadi. Utafiti huu ulifuata maadili ya utafiti na uliongozwa na nadharia mbili ambazo ni nadharia ya kijamii na nadharia ya utekelezaji. Katika nadharia ya utekelezaji na nadharia ya kijamii tunaona hizi zinatoa mwongozo wa umuhimu wa kutumia lugha inayozungumzwa na watu wengi ndani ya jamii na madhara ya kutumia lugha isiyozungumzwa na watu wengi. Uteuzi wa lugha inayozungumzwa na watu wengi huipa dhima ya kitaifa, Kwa mfano, lugha ya kujifunzia na kufundishia ni kipengele kimojawapo cha uendelezaji wa mila, desturi na utamaduni wa jamii moja kwenda jamii nyingine na iwapo jamii itapuuza matumizi ya lugha inayotumiwa na watu wengi ipo hatari ya kupoteza ustaarabu, mila, desturi na utamaduni wake. Katika utafiti huu, mtafiti aligundua kuwa tamko la sera ya elimu na mafunzo kuhusu kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu katika vyuo vya kati lipo bayana na linatoa mwelekeo mpya wa fikra za kimapinduzi katika mfumo wa elimu nchini Tanzania. Hata hivyo, tamko hilo halionyesha lini litaanza kutumika. Pia jamii haijaelimishwa juu ya umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia ndiyo maana baadhi ya watafitiwa hawana ufahamu juu ya uwepo wake. Kuwepo kwa tamko hilo katika sera ya elimu, pia katika katiba pendekezwa ya nchi kuwa Kiswahili ni moja ya tunu za taifa kumeibua mjadala upya wa umuhimu wa Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia.

Aidha, utekelezaji wa sera ya elimu kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia vyuo vya kati bado haijapewa kipaumbele. Hii inatokana na kuwepo na changamoto mbalimbali kama vile kukosekana kwa taratibu na kanuni zitakazosimamia utekelezaji, hofu ya wadau kupokea mabadiliko, jamii haijaandaliwa kupokea mabadiliko, ufinyu wa bajeti ya serikali na kutoundwa kwa vyombo vitakavyosimamia utekelezaji. Hivyo kuwepo kwa changamoto hizo kunachangia kusuasua kwa utekelezaji wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati.

5.3 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na madhumuni mahsusi matatu kama yalivyobainishwa katika sehemu 3.1 na 5.2. Kwa kutumia data zilizopatikana kwa watafitiwa kupitia mbinu ya usaili na hojaji.

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa, tamko la sera ya elimu na mafunzo kuhusu kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu katika vyuo vya kati lipo bayana na linatoa mwelekeo mpya wa fikra za kimapinduzi katika mfumo wa elimu nchini Tanzania. Hata hivyo tamko hilo halionyesha lini litaanza kutumika. Pia jamii haijaelimishwa juu ya umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia ndiyo maana baadhi ya watafitiwa hawana ufahamu juu ya uwepo wake. Kuwepo kwa tamko hilo katika sera ya elimu, pia katika katiba pendekezwa ya nchi kuwa Kiswahili ni moja ya tunu za taifa kumeibua mjadala upya wa umuhimu wa Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia.

Madhumuni mahsusi ya pili ya utafiti huu yalikuwa kubainisha changamoto za utekelezaji wa sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia na kutoa mapendekezo juu ya utekelezaji juu ya sera ya elimu kuhusu matumzi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia. Matokeo ya utafiti huu yamebaini changamoto ya msingi ya utekelezaji wa matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu katika vyuo vya kati. Changamoto hizo ni pamoja na sera kutokuwa na nguvu za kisheria kwani Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haijatamka waziwazi matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati. Changamoto ya pili, jamii haijaelimishwa maana na umuhimu wa kutumia lugha yao ya Kiswahili katika kujifunzia na kufundishia elimu katika vyuo vya kati badala yake jamii huona kujua Kiingereza ndiyo kuelimika kwa sababu mtu anayeongea Kiingereza huonekana ndiye msomi kuliko yule anayeongea Kiswahili. Changamoto la tatu, ni hofu ya viongozi na washika dau walio katika vyombo vya maamuzi kuwa nchi ikiacha lugha ya Kiingereza na kutumia Kiswahili itakuwa kisiwa. Changamoto ya nne, ni uchumi tegemezi wa nchi unakwamisha kufanya mabadiliko ya lugha ya kufundishia na kujifunzia kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili kwa kuwa kunahitajika gharama za kifedha na kitaalamu kufanikisha mabadiliko yenye tija. Changamoto ya tano, kutokuundwa kwa vyombo maalumu vya kusimamia utekelezaji wa sera ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati. Changamoto ya sita, ni kasumba ya kuona kuwa lugha ya Kiswahili haina istilahi za kutosha kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati.

Madhumuni ya tatu yalikuwa kutoa mapendekezo juu ya utekelezaji wa sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia. Matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa, lugha inayotumika kwa sasa inaathiri wa elimu inayotolewa katika vyuo vya kati. Baadhi ya wanachuo na walimu wengi hawana umahiri na uweledi wa kutosha wa kutumia lugha ya Kiingereza, hivyo huwalazimu walimu na wanachuo kubadili msimbo katika kufafanua dhana na kurahisisha mawasilino katika ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, baadhi ya wanachuo hutatizwa na lugha inayotumika katika kujifunza au kufundishia na kusababisha kupata ufaulu usio ridhisha katika kozi wanazosoma. Vilevile, baadhi ya wataalamu wanaohitimu katika vyuo vya kati hawanana umahiri na uweledi wa kutumia kwa usahihi na ufasaha lugha ya Kiingereza ama Kiswahili. Pia, kutofikiwa kwa muafaka wa mjadala wa muda mrefu unaoendelea juu ya lugha ipi itumike katika ujifunzaji na ufundishaji wa elimu ya juu kwa mustakabali wa taifa hili.

Kwa hiyo, Utafiti huu ulipendekeza matumizi ya lugha ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya kati. Vilevile, kuipa kanuni na taratibu za utekelezaji sera ya elimu na mafunzo juu ya matumizi ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu katika vyuo vya kati. Kwa kufanya hivyo taifa litaweza kuinua ubora wa elimu kwa kuwapa wakufunzi, wanachuo na jamii lugha inayoeleweka katika kufundisha na kujifunza.

5.4 Mapendekezo

Kimsingi lugha ya kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati ndiyo inayotoa mchango mkubwa kwa jamii, kwa vile lugha hubeba utamaduni, mila na

ustaarabu wa jamii. Kutokana na maelezo hayo, utafiti huu unatoa mapendekezo yafuatayo:

Kwanza, katiba ya nchi itamke wazi kuwa Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia na kujifunzia elimu katika vyuo vya kati, kwa vile lugha ya Kiswahili inazungumzwa na Watanzania wengi. Kwa kufanya hivyo, kutasaidia Kiswahili kutungiwa kanuni zitakazosimamia mwendelezo wa utekelezaji wa tamko la lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia na kujifunzia elimu katika vyuo vya kati hapa Tanzania.

Pili, kuwapo kwa maamuzi ya dhati yasiyo na kigugumizi juu ya kutumika lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya vyuo vya kati. Hii itasaidia wanachuo kuongeza uwezo wao wa kuelewa masomo wanayojifunza na kuwajengea umahiri na uweledi katika lugha na fani wanazojifunza kwa vile watasoma kwa lugha waliyoizoea na ambayo wataitumia watakapo kuwa wanawahudumia Watanzania na watu wa mataifa mengine watumiao Kiswahili.

Tatu, kuondoa vizuizi vya kutumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu ili kuwezesha wanachuo kupata fursa ya kujifunza taaluma zao kwa kutumia lugha ya Kiswahili, lugha ambayo huitumia kwa kiwango kikubwa katika kuwahudumia Watanzania wa kada mbalimbali.

Nne, utafiti huu unapendekeza kuwa viongozi na wanasiasa wenye dhamana ya masuala ya lugha waelimishwe kuhusu umuhimu wa lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia elimu katika vyuo vya kati ili waridhie katika akili zao na

kuwa mawakala wazuri wa kuwaelimisha raia, kwa vile wao ndio wenye dhamana ya kufanya maamuzi. Viongozi na wanasisia wakielimishwa na kuelewa umuhimu walugha ya Kiswahili watasaidia sana katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Tanzania.

Tano, maandalizi ya dhati ya kisaikolojia, kiuchumi na kijamii yanahitajika ili kuwafanya Watanzania wabaini kuwa hakuna lugha bora kuliko nyingine. Hivyo, Kiswahili kama lugha zingine kikipewa fursa katika mfumo wa elimu kinao uwezo wa kutolea maarifa na ujuzi kwa wanataaluma wa ngazi mbalimbali.

Sita, jamii ielimishwe umuhimu na uwezo iliyonayo lugha ya Kiswahili katika kufanikisha malengo ya elimu kwa jamii nzima kwa ufanisi na usawa.

5.5 Maeneo Yanayohitaji Utafiti Zaidi

Utafiti unatoa mapendekezo juu ya mada ambazo zingefanyiwa utafiti na watafiti wajao. Maeneo hayo ni haya yafuatayo:

- i) Kutathimini sababu zinazofanya lugha ya Kiswahili kutotumika kufundishia elimu ya juu nchini Tanzania.
- ii) Kuchunguza sababu za kutokuwapo kwa sera kamilifuya lugha inayojitegemea nchini Tanzania.
- iii) Kubaini sababu za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokutamka bayana juu ya lugha ya Kiswahili kutumika katika kujifunzia na kufundishia elimu kwa ngazi zote.

5.6 Hitimishi

Sura hii imeeleza kwa muhtasari utafiti unaohusu “kuchunguza mtazamo wa jamii juu ya sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka (2014) kuhusu matumizi ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Kati.” Katika sura hii tumeeleza malengo ya utafiti, mbinuzilizotumiwa kukusanya data, eneo ambapo utafiti umefanyika pamoja na nadharia zilizotumika katika kuchambua data. Aidha, uchambuzi wa data umeelezwa na matokeo ya utafiti kubainishwa kwa ufasaha. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, mtazamo wa jamii juu ya sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka (2014) kuhusu matumizi ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Kati, ni kuwepo kwa manufaa makubwa katika ubora wa elimu itakayotolewa katika vyuo vya kati, hata hivyo serikali haijatoa kipaumbele katika matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia kwa kuwa haijatoa tamko rasimi ambalo litaagiza utendaji na utekelezaji wa matumizi ya Kiswahili katika mfumo wa elimu. Pia katika utafiti huu mtafiti amethibitisha athari zitokanazo na uwili lugha katika utoaji wa taaluma na mafunzo. Aidha, mapendekezo ya maeneo yanayohitaji utafiti zaidi yamefanyika

MAREJELEO

- Bamgbose, A. (1991). *Language and the Nation: the Language Question in Sub Sahara Africa*. Edinburgh: Edinburgh Press.
- Bernstein, B. (1977). *Class, Code and Control*. London: Routledge.
- Bhaiji, A. F. (1976). *The Medium of Instruction in Our Secondary Schools*. A Study report in Education and Development. Department of Education, University of Dar es Salaam. Dar es Salaam, Tanzania.
- Bourdier, P. & Passeron, J. (1977). *Reproduction –Education, Society and Culture*. London: SAGE Publications Ltd.
- Brock-Utne, B. & Wenzake, (eds). (2003). *Language of Instruction in Tanzania and South (LOITASA)*. Dar es Salaam: E & D Publishers.
- Brock-Utne, B. (2001). The most Recent Developments concerning the Debate on language of instruction in Tanzania. Paper Presented to the NETREED conference from 7th to 9th January. Institute of educational Research, University of Oslo, Sweden. Retrieved on 12th March, 2017 from www.netreed.uio.no/conferences/Brock-Utne.doc.
- Brock-Utne, B. (2002). *Whose Education for all? The recolonization of the African Mind*. New York: Falmer Press.
- Brock-Utne, B. (2005). Learning through a familiar language versus learning through a foreign language: A look into some Secondary School Classroom in Tanzania. *International Journal of Educational Development*, 27(5), 487–498. Retrieved from <https://www.sensepublishers.com/.../567-language-of-instruction-in-tanzania-and-sout> on 11th May, 2016.

- Brock-Utne, B. (2005). *The Continued Battle over Kiswahili as the Language of Instruction in Tanzania*. In Brock –Utne, Birgit & Hopson, Rodney Kofi. *Language of Instruction for Africa emancipation: Focus on Post Colonial Context Considerations*. Dar es Salaam: Mkuki & Nyota Publishers.
- Burchert, L. (1997). *Education Policy Formulation Tanzania coordination between the Government and International Aid Agencies*. Paris: International Institute for Educational Planning.
- Coulmas, F. (Eds), (1989). *Language Adaption*. Cambridge University Press. Cambridge.
- Criper, C. & Dodd, W. (1984). *Report on the Teaching of English language and its use as a medium of Education in Tanzania*. The British Council. Dar es Salaam, Tanzania.
- Desai, Z. & Qorro, M. (Eds.). *LOITASA Research in Progress*. Dar es Salaam: KAD Associates.
- Fishman, J. A. (1972). *Sociolinguistics*. Massachusetts: Newbury House Publishers.
- Giglioli, P. (1972). *Language and Social Context*. Middlesex: Penguin Books.
- Gottneid, A. J. (Ed). (1976). *Church and Education in Tanzania*. Nairobi: East African Publishing.
- Halliday, M. A. K. (1973). *Exploration in the Function of Language*. London: Edward Arnold.
- Kaplan, R. B. & Baldauf, R. B. (1977). *Language Planning: From Practices to Theory*. Clevedon: Multilingua matters.

- Kiango, J. G. (1999). *Uteuzi wa lugha kwa ajili ya Elimu* katika Z. N. Tumbo Masabo & E. E. F. K. Chiduo (Wahariri) *Kiswahili katika Elimu*. Dar-es-Salaam: TUKI.
- Kiango, J. G. (2002). Nafasi ya Kiswahili katika Ujenzi wa Jamii Mpya: *Nordic Journal of African Studies* 11(2), 185-197. Imepakuliwa tarehe 13 Mei, 2017 kutoka www.njas.helsinki.fi/abstracts/vol11num2/abstract_11_2_3.html.
- Kombo, D. K. & Tromp, D. L. (2006). *Proposal and Thesis writing; An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology Methods and Technique* (Second Revised Edition). New Delhi: New Age International Publishers.
- Kothari, C. R. (2011). *Research Methodology: Methods and Techniques* (Second Revised Edition), New Delhi: New Age International Publishers.
- Mekacha, R. D. K. (2000). *Isimu jamii: Nadharia na Mukadha wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mhina, G. (1972). *Another Language Gap that Awaits Policy Decision*. Unpublished Paper. Dar-es Salaam, Tanzania.
- Mkwizu, M, A. (2003). The Pedagogical Implication of Using English as the Medium of Instruction in Teaching Civics in Tanzania Secondary Schools. Unpublished Master thesis. University of Oslo, Sweden. Retrieved on 25th April, 2017 from www.linse.uni-due.de/.../.
- Mlama, P. & Matheru, B. (1978). *Haja ya Kutumia Kiswahili Kufundishia katika Elimu ya juu*. Dar es Salaam: BAKITA.
- Mligo, E. S. (2012). *Jifunze Utafiti: Mwongozo Kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti Yenye Mantiki*. Dar es Salaam: Ecumenical Gathering (EGYS).

- Morrison, A. (1971). *School and Socialization*. Harmondsworth: Penguin Books Ltd.
- Mpemba, T. (2007). Tanzania Policy Makers. Reluctance to Sanction Kiswahili instructional medium in post primary Education. How do Learners and Instructors Cope with or Resist the English medium policy? University of Dar es Salaam, Dar es Salaam. (Tasnifu isiyochapishwa ya M.A Kiswahili).
- Msanjila Y. P. (2009). *Haja ya Kuwa na Sera Toshelevu ya Lugha Tanzania: Uzoefu na Changamoto*” katika *Mulika* Na. 28, 62-71.
- Msanjila, Y. P, & Wenzake, (2009). *Isimu Jamii: Sekondari na Vyu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Msanjila, Y. P. & Wenzake (2011). *Isimu Jamii Sekondari na Vyu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Msanjila, Y. P. (2003). *Kushuka kwa Hadhi ya Lugha za Jamii Nchini Tanzania. Nordic Journal of Africa studies*, 12(3), 296 - 309. Imepakuliwa tarehe 12 Machi, 2017 kutoka www.njas.helsinki.fi/pdf-files/vol12num3/msanjila.pdf.
- Msanjila, Y. P. (1998). Uzoefu wa kutumia Kiswahili kama Lugha ya kufundishia katika Vyu vya Ualimu nchini Tanzania. *Journal of Linguistics and Language in Education*, 3, 75-95. Imepakuliwa tarehe 5 Juni, 2017 kutoka ir-library.ku.ac.ke/bitstream/.../Nadharia%20za%20Uhakiki....pdf.
- Neuman, N. L. (2006). *Social Research* (6th Edition). Boston: Pearson Publisher.
- Peterson, R. (2006). The Use of an African Language as Language of Instruction at University level: The example of Kiswahili Department at the University of Dar es Salaam in Tanzania. Unpublishe Master of Philosophy Studies, University of Oslo, Oslo, Sweden. Retrieved on 22nd March, 2017 from

<https://www.duo.uio.no/bitstream/handle/10852/30791/1/correctedxversionxorxCIEExdissertation.pdf>.

- Powell, R, Conway, C. & Lynda, R. (2004). Effects of Student Predisposing Characteristics on Student Success, *Journal of Distance Education*, 5(1), 20-37. Retrieved from ijede.ca/index.php/jde/article/view/368/259 on 7th July, 2016.
- Prah, K. K. (2003). *Going Native: Language of instruction for Education, Development and African Emancipation*. In B. Brock Utne, Z Depai and Qorro. (Eds). *Languages of instruction in Tanzania*. Dar-es Salaam: E & D Limited.
- Qorro, M. A. S. (2006). Does language of Instruction Affect Quality of Education? Haki Elimu working papers. Dar es Salaam, Tanzania.
- Rubagumya, C. M. (1996). *Research Tells Us about Language of Instruction in Tanzania*, Nairobi: IDRC.
- Rubanza, Y. (2000). *The Question of medium of instruction*. In Galabawa, Justin, F. E. M. K Senkoro and A. F. Lwaitama (Eds) *The Quality of Education in Tanzania Issues and Experiences*. Dar-es Salaam: DUP.
- Rubanza, Y. I. (2002). *Realistic Revolutionary Strategies in Harmonisation and Standardisation of African Language*. In, Kwes Kwaa Prah (eds) *Rehabilitating African Languages*. Cape Town: CASAS.
- Rubin, J. & Jenudd, B. H. (Eds) (1971). *Can Language be planned? Sociolinguistic Theory and Practice for Developing Nations*. Honolulu: Honolulu University Press.

- Sengo, T. S. Y. M. K. S. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: AERA Kiswahili Researched Product.
- Senkoro, F. (2004). Teaching in Kiswahili at the University Level: The case of Kiswahili Department at the University of Dar es salaam. Paper presented at LOITASA International conference on Language of Instruction in Education 26- 27 January. Arusha, Tanzania.
- Sigh, K. (2007). *Quantitative Social Research Method*. New Delhi: Routledge Taylor & Francis Group.
- Speziale, H. S. & Carpenter, D. R. (2006). *Qualitative research in Nursing: Advancing the Humanistic Imperative*. Philadelphia: Lippincott Williams and Wilkins.
- Swilla, I. N. (2009). Language of Instruction in Tanzania. Contradiction between Ideology Policy and Impementation. *African Study Monographs* 30 (1), 1–14. Retrieved from <https://books.google.co.tz/books?isbn=1136165827> on 23rd September, 2016.
- Tumbo-Massambo, E. N & Chiduo, E. K. F. (Wah.), (2007). *Kiswahili Katika Elimu*. Dar es Salaam: TUKI.
- UNESCO, (1953). *The Use of Vernacular Languges in Education*, Paris.
- United Republic of Tanzania, (1984). *Educational System in Tanzania towards the Year 2000: Recommendation of the 1982 Presidential Commission on Education*. Ministry of Nation Education. Dar es Salaam, Tanzania.
- United Republic of Tanzania, (1985). *Basic Education Statistics in Tanzania 1980-1984*. Dar es Salaam, Tanzania.

- Whitely, W. (1969). *Swahili: The rise of National Language*. London: Methuen and Co. Ltd.
- Williman, N. (2011). *Research Methods: The Basic*. London & NewYork: Routledge.
- Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, (2014), *Sera ya Elimu na Mafunzo*. Dar-es Salaam, Tanzania.
- Wizara ya Elimu na Utamaduni, (1997). *Sera ya Utamaduni*. Dar-es Salaam, Tanzania.
- Yin, R. K. (1994). *Case Study Research: Design and Methods* (2nd eds). Thousand Oaks California: SAGE Publishers.
- Yorad, S. Y. (2011). *Lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu shuleni na vyuo vya Ualimu: Tasnifu ya Uzamili (M.A Kiswahili) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania*.

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho A: Hojaji kwa Wanachuo

Hojaji hii ni kwa ajili ya utafiti unaohusu “Mtazamo wa Jamii juu ya sera ya elimu na mafunzo 2014 Kuhusu Kutumia Kiswahili Kufundishia na Kujifunzia Elimu ya Juu katika Vyuo vya Kati.”

Tafadhali jibu maswali haya kwa mujibu wa uelewa wako na kwa usahihi ili usaidie kutoa matokeo yakinifu yatakayochangia katika kukamilisha utafiti huu. Majibu ya maswali utakayoyatoa yatakuwa siri baina ya mtafiti na mtafitiwa.

SEHEMU A: TAARIFA BINAFSI

- (i) Unasoma mwaka wa ngapi?.....
- (ii) Jinsi yako.....
- (iii) Kozi unayofundisha.....
- (i) Kiwango cha elimu.....
- (iii)Uzoefu kazini.....

SEHEMU B:

1. Je, umewahi kusikia/kusoma tamko la kutumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati? Ndiyo/Hapana.

Kamandiyolinasisitiza nini?

.....

2. (a) Sera ya elimu na mafunzo kuhusu kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati ,Je iko wazi kwa kuisoma na kuelekwa kwa wadau wote wa elimu? Ndiyo/Hapana.

(b) kama jibu ni hapana toa sababu za jibu lako (swali 2a).

.....
.....
.....

(c) Kama jibu ni ndiyo, Jeinatekelezeka?

.....
.....
.....

3.Je,kuna hatua zozote zilizokwisha chukuliwa na serikali kuhakikisha Kiswahili kinatumika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati? Ndiyo/Hapana

Kama jibu ni ndiyo,hatua hizo ni zipi?.kamajibu ni hapana kwanini?

.....
.....
.....

4. Je,Kuna mikakati yoyote ya utekelezaji iliyowekwa na serikali katika kufikia azma yake ya kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati? Ndiyo/Hapana

Kama ndiyo taja mikakati hiyo: -

.....
.....

5. (a) Je, lugha ya Kiswahili ikitumika katika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati, kuna shida? Ndiyo/Hapana.

(b) Toa maoni yako kuhusu jibu lako (swali la 5a)

.....
.....
.....

6. Je, unapendelea kutumia lugha gani zaidi katika mijadala/majadiliano ya mada za masomo unayofundishwa hapa chuoni kati ya lugha zifuatazo; -

(i) Kiingereza

(ii) Kiswahili

(b) Eleza sababu za kupendelea lugha hiyo (swali la 6a)

.....
.....
.....

7 (a) Je, unafikirilugha unayotumia katika kujifunzia mada za masomo ya fani yako ina mchango wowote katika kueleweka kwa mada na ufaulu wa wanachuo? Ndiyo/Hapana.

b) Eleza sababu za jibu lako (swali la 7a)

.....
.....
.....

8 Taja changamoto zilizopo katika utekelezaji wa sera ya elimu na mafunzo 2014 kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia.

.....
.....
.....

9. (a) Kwa maoni yako, Je kuna manufaa ya lugha ya Kiswahili kutumika kama lugha ya kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati? Ndiyo/Hapana

(b) Eleza sababu za jibu lako (swali la 9a)

.....
.....
.....

10. Je, ni kwa kiwango gani lugha ya kufundishia inayotumika kwa sasa inaatahiri ubora wa mafunzo yanayotolewa katika vyuo vya kati.?

.....
.....
.....

11. Je, kuna athari zozote zitokanazo na kutotekelezwa kwa tamko la matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati? Ndiyo/Hapana.

(b) Toa maelezo ya jibu lako.

.....
.....
.....

ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO

Kiambatanisho B: Hojaji kwa Wakufunzi

Hojaji hii ni kwa ajili ya utafiti unaohusu “Mtazamo wa Jamii juu ya sera ya elimu na mafunzo 2014 Kuhusu Kutumia Kiswahili Kufundishia na Kujifunzia Elimu ya Juu katika Vyuo vya Kati.”

Tafadhali jibu maswali haya kwa mujibu wa uelewa wako na kwa usahihi ili usaidie kutoa matokeo yakinifu yatakayochangia katika kukamilisha utafiti huu. Majibu ya maswali utakayoyatoa yatakuwa siri baina ya mtafiti na mtafitiwa.

SEHEMU A: TAARIFA BINAFSI

- (i) Unafundisha wa mwaka wa ngapi?
- (ii) Jinsi yako.....
- (iii) Kozi unayofundisha.....
- (ii) Kiwango cha elimu.....
- (iv) Uzoefu kazini.....

SEHEMU B:

1. Je, umewahi kusikia/kusoma tamko la kutumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati? Ndiyo/Hapana. Kamandiyolinasisitiza nini?
.....
.....
2. (a) Sera ya elimu na mafunzo kuhusu kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati, Je iko wazi kwa kuisoma na kuelekwa kwa wadau wote wa elimu? Ndiyo/Hapana.

(b) kama jibu ni hapana toa sababu za jibu lako (swali 2a).

.....
.....
.....

(c) Kama jibu ni ndiyo, Jeinatekelezeka?

.....
.....
.....

3. Je, kuna hatua zozote zilizokwisha chukuliwa na serikali kuhakikisha Kiswahili kinatumika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati?

Ndiyo/Hapana

Kama jibu ni ndiyo, hatua hizo ni zipi? kamajibu ni hapana kwanini?

.....
.....
.....

4. Je, kuna mikakati yoyote ya utekelezaji iliyowekwa na serikali katika kufikia azma yake ya kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati? Ndiyo/Hapana

Kama ndiyo taja mikakati hiyo: -

.....
.....
.....

5. (a) Je, lugha ya Kiswahili ikitumika katika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati, kuna shida? Ndiyo/Hapana.

(b) Toa maoni yako kuhusu jibu lako (swali la 5a)

.....
.....
.....

6. Je, unapendelea kutumia lugha gani zaidi katika mijadala/majadiliano ya mada za masomo unayofundisha hapa chuoni kati ya lugha zifuatazo; -

(i) Kiingereza

(ii) Kiswahili

(b) Eleza sababu za kupendelea lugha hiyo (swali la 6a)

.....
.....
.....

7 (a) Je,unafikirilugha unayotumia katika kufundishia mada za masomo ya fani yako ina mchango wowote katika kueleweka kwa mada na ufaulu wa wanachuo? Ndiyo/Hapana.

b) Eleza sababu za jibu lako (swali la 7a)

.....
.....
.....

8 Taja changamoto zilizopo katika utekelezaji wa sera ya elimu na mafunzo 2014 kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia.

.....
.....
.....
.....

9. (a) Je, kwa maoni yako kuna manufaa yoyote ya lugha ya Kiswahili kutumika kama lugha ya kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati. Ndiyo/Hapana

(b) Eleza sababu za jibu lako (swali la 9a)

.....
.....
.....

10. Je, ni kwa kiwango gani lugha ya kufundishia inayotumika kwa sasa inaathiri ubora wa mafunzo yanayotolewa katika vyuo vya kati.?

.....
.....
.....

11. Je, kuna athari zozote zitokanazo na kutotekelezwa kwa tamko la matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati?. Ndiyo/Hapana.

(b) Toa maelezo ya jibu lako.

.....
.....
.....

ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO

Kiambatanisho B: Mwongozo wa Usaili kwa Wataalamu na Wadau wa Elimu

Utangulizi:

Mimi ni Mwanafunzi wa Shahada ya Uzamilia (M.A. Kiswahili) katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Ninafanya Utafiti wenye anwani isemayo: **“Mtazamo wa Jamii juu sera ya elimu na mafunzo 2014 Kuhusu Kutumia Kiswahili Kufundishia na Kujifunzia Elimu ya Juu katika Vyuo vya Kati.”**

Naomba nikushirikishe katika Utafiti huu kwa kukufanyia Usaili. Napenda kukuhakikishia kuwa taarifa zote utakazonipa zitahifadhiwa katika hali ya usiri na kutumika kwa madhumuni ya elimu tu.

Sehemu A: Taarifa binafsi

- (i) JinaJinsi.....
- (ii) Kiwango cha Elimu
- (iii) Kazi yako
- (iv) Uzoefu wako kazini ni miaka

Sehemu B; Maswali

1. Je, umewahi kulisikia ama kulisoma tamko la matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu?

.....

2. Je, sera ya elimu na mafunzo kuhusu kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati iko wazi kwa wadau wote wa elimu?

.....
.....

3. Je, kuna hatua zozote zilizokwisha chukuliwa na serikali katika kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inatumika kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati?

.....
.....
.....

4. Je, kuna mikakati yoyote unayoifahamu ambayo imewekwa na serikali katika kutekeleza sera ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu katika vyuo vya kati? Ndiyo/hapana kama ndiyo itaje.

.....
.....

5. (a) Je, lugha ya Kiswahili ikitumika kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya kati kuna shida?

(b) Toa maoni kuhusu jibu lako (swali 5a).

.....
.....
.....

6. (a) Je, unafikiri yanaweza kutokeamatatizo gani katika utekelezaji wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia katika elimu ya juu katika vyuo vya kati?

.....
.....

(b) Nini kifanyikeili kuondokana na matatizo hayo?

.....
.....
.....

7. Je, ni kwa kiwango gani lugha ya kufundishia na kujifunzia inayotumika sasa katika vyuo vya kati inaathiri ubora wa elimu na mafunzo yanayotolewa.

.....
.....
.....

8. Kuna athari zipi zitokanazo na kutotekelezwa kwa tamko la matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati. Toa sababu kwa athari hizo.

.....
.....
.....

Maoni yako ni yapi kuhusu kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo

.....
.....
.....

ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO

Kiambatanisho D: Ufafanuzi wa Dhana Na Vifupishi Katika Utafiti

- (i) Sera ya lugha – maandishi kuhusu jinsi lugha zinavyopaswa kutumika katika jamii yaani, lugha ipi itumike katika maeneo yapi?
- (ii) Mtazamo- ni fikra au muono wa mtu juu ya jambo fulani katika jamii
- (iii) Lugha ya kwanza – huwakilisha lugha mama, lugha ya jamii katika jamii kubwa.
- (iv) Vyuo vya Kati – Vyuo visivyo vyuo vikuu, ambavyo hutoa vyeti vya mafunzo ya wahitimuwa kidato cha nne na cha sita.
- (v) ADEM- Agency for the Development of Educational Management (Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu).
- (vi) CBE-College of Business Education (Chuo cha elimu ya Biashara)
- (vii) LOITASA- Language of Instruction in Tanzania and South Africa.
- (viii) TUKI-Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili